epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumatatu Novemba 18, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581864

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

GHOROFA LILILOPOROMOKA

# Vigogo matumbo joto



• **Rais** Samia aagiza mmiliki ahojiwe, uchunguzi majengo yote Kariakoo... *ukurasa 2*

UKURASA WA 7

**Serikali** yashauriwa kurekebisha mfumo mpya wa mikopo kwa watumishi

UKURASA WA 8

**Profesa** Janabi: Wekeza kwenye afya, siyo mali

UKURASA WA 17

**Bodaboda** chanzo cha ongezeko la ajali barabarani Zanzibar



UK. 3

## Hatimaye Makonda afunguka shambulio la Lissu, uvamizi wa studio Clouds Media



Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu (wa tatu kushoto), akizindua Ilani ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongozi ya chama hicho 2024-2029 wakati wa hafla maalumu iliyofanyika ofisi za Makao Makuu, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT kukimbilia kortini kupinga wagombea kuenguliwa S/Mitaa

• **CCM**, CHADEMA 'weka tuweke' miji ya kimkakati... ...*Uk. 3 & 4*

Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu

**MICHEZO** **RAMOVIC ATAMBA KUIFAHAMU SIMBA** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Vigogo matumbo joto uchunguzi Kariakoo

**Na Waandishi Wetu**

USALAMA wa majengo yaliyoko Kariakoo, jijini Ilala umeibua jambo, wamiliki wake wako matumbo joto:

Rais Samia Suluhu Hassan amemwagiza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuongoza timu ya wakaguzi majengo kukagua majengo yote yaliyoko eneo hilo la kibiashara ili kujua hali ilivyo katika majengo hayo.

Alitoa maelekezo hayo jana wakati akizungumza na watanzania akiwa jijini Rio de Janeiro, Brazil ambako amekwenda kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Nchi Wanachama wa Kundi la G20.

Rais Samia pia ameliagiza Jeshi la Polisi kupata taarifa kamili kwa mmiliki wa jengo lililoporomoka jinsi ujenzi ulivyokuwa unafanyika.

"Baada ya zoezi la uokoaji kukamilika, ninamtaka Waziri Mkuu aongoze timu ya wakaguzi majengo waendelee na zoezi la kukagua majengo yote ya Kariakoo na kupata taarifa kamili ya hali ya majengo ya Kariakoo," Rais Samia aliagiza.

Alisema serikali itahakikisha inatoa ushirikiano kuanzia mwanzo wa zoezi hili hadi mwisho na kwamba taarifa za uchunguzi zitakapopatikana, zitawekwa wazi na hatua zitakazochukuliwa na serikali zitawekwa wazi pia.

Mkuu wa Nchi alisema kuwa kwa mujibu wa taarifa alizopewa, hadi kufikia saa 4:00 asubuhi watu waliokuwa wameokolewa ni 84 na kati yao, majeruhi 26 walikuwa wanaendelea na matibabu hospitalini na watu 13 wamefariki dunia kutokana na kuporomoka kwa ghorofa hilo.

Aliongeza kuwa serikali itagharamia matibabu na kuvipongeza vyombo vya ulinzi na usalama, mashirika mbalimbali, wananchi na madaktari wanaowahudumia majeruhi.

**MANUSURA ASIMULIA**

Mmoja wa manusura wa tukio hilo, Hassan Yahya, ameelezea namna walivyotumia fimbo kuomba msaada wa kuokolewa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini, Yahya alisema kuwa katika eneo walikokuwa wamenasa, walibaini kuwapo upenyo wenye nafasi ndogo na hivyo wakawa wamebahatisha kupata fimbo ambayo waliitumia kuomba msaada.

"Mimi ni mfanyabiashara katika jengo lililoporomoka, na mpaka linadondoka, nilikuwa ghorofa ya katikati. Nikiwa humo, nilisikia mtikisitiko mkubwa, ghafla nikaona majirani zangu wanakimbia, ikabidi na mimi nikimbie kuwafuata, nikawaza kwamba kuna jambo haliko sawa.

"Wakati ninakimbia, wala sikufika mbali, tukawa tumekutana watu wengi kama 26, hivi kwenye hicho kieneo, kila mtu anataka kutoka, kila mtu analia, ikabidi tuteue viongozi wa kudhibiti hiyo hali, nikajiteua mwenyewe kuongoza.

"Tukaanza kuulizana kila mmoja na kuhangaika kutafuta sehemu hata kunakopatikana mwanga hata kidogo, tukafanikiwa kupata kiupenyo kidogo ambacho hata mkono hauwezi kupita, tukatumia kifimbo ambacho tulikiokota kukapenyeza hapo kuomba msaada kwa waokoaji, ndipo wakawa wametuona, wakaanza kuvunja ukuta.

"Tulikubaliana kwamba waanze watoto watolewe na mimi nilikuwa wa tatu mwishoni kutoka katika lile kundi letu, lakini wakati huo tulikuwa tunasikia na wenzetu upande mwingine wanaomba msaada," alisema Yahya.



Alisema kwamba alipopata uhakika wa kutolewa, yeye na wenzake wawili waliokuwa wa mwisho, walipiga picha na kisha kuituma kwa ndugu zao kuwataarifu kwamba wako hai.

Pia alisema kuwa baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini Muhimbili alikokuwa amepelekwa, alipokea simu nyingi za watu waliokuwa wamepata taharuki kwamba amefariki dunia.

Akiwa eneo la tukio jana, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (CGF), John Masunga, alisema waliwasiliana na baadhi ya watu ambao wako chini ya jengo hilo wakiwaambia kuwa wako salama.

Kamishna Masunga alisema kuwa baadhi yao walichukua hatua ya kugonga kuta kama ishara ya kuwaonesha mahali walipo ili wawapatie msaada.

"Pamoja na kufanikiwa kuwaokoa baadhi ya watu waliofukiwa na kuwapatia huduma ya Oksijeni, maji na glucose, tumekutana na changamoto nyingi, hivyo kulazimika kuvunja kuta mbilimbili hadi tatu ili kuwafikia walioko chini, tulitumia mbinu ya kutoboa mashimo kwa haraka ili tuwapatie huduma lakini pia kuwafikia," alisema Kamishna Masunga.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alitoa taarifa kuwa, watu 77 walikuwa wameokolewa huku watano wakifariki dunia.

Naibu Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Dar es Salaam, Renatus Mlelwa, alisema ameridhishwa na kazi kubwa inayoendelea kufanywa na timu ya wataalamu wa uokoaji.

Nipashe ilishuhudia ulinzi katika eneo hilo na maeneo mengi ya Kariakoo ukiwa umeimarishwa.

Vikosi vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Wananchi (JWTZ), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) vilikuwa vimetanda katika eneo hilo na eneo kubwa la Kariakoo kuimarisha ulinzi.

**BALOZI NCHIMBI**

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi alipongeza utayari na mshikamano uliooneshwa na watanzania baada ya tukio la kuanguka kwa jengo hilo, akisema kuwa hatua hizo zimeonesha uzalendo na moyo wa udugu uliojengwa ndani ya taifa.

Baada ya kutembelea eneo la tukio jana, Balozi Nchimbi alitoa pole kwa familia za waliopoteza maisha na kuwapa faraja waliojeruhiwa, huku akisisitiza umuhimu wa mshikamano katika nyakati za dharura.

"Kwa namna ya pekee, ninapenda kutoa pole zangu za dhati kwa familia za wenzetu waliopoteza maisha. Maisha ya kila mtanzania yana thamani kubwa.

"Kwa walioumia, walioko hospitalini na hata waliotoka, tunawaombea uponaji wa haraka. Mwenyezi Mungu awajalie nguvu na afya njema ili mrejea katika shughuli zenu," alisema.


Katika hotuba yake, Balozi Nchimbi alipongeza serikali na vyombo vyake, hasa Wizara ya Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), pamoja na timu zake zikiongozwa na Waziri William Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, na taasisi mbalimbali zilizoonesha mshikamano wa dhati katika kuhakikisha maisha yanaokolewa.

"Serikali inafanya kazi yake kwa ufanisi. Hiki ndicho tunachotarajia kutoka kwenye serikali za CCM–kuwa na uwapo wa karibu wakati wa matatizo. Ninawashukuru wote mnaoendelea kuwa hapa kushughulikia hali hii kwa ari kubwa," alisema.

Aliongeza kuwa juhudi za vyombo vya ulinzi na usalama, taasisi binafsi na wadau wengine zinapaswa kupongezwa kwa moyo wa kujitolea.

"Uokoaji huu haupaswi kusimama. Kila maisha yanahesabika. Kama chama, tupo tayari kushirikiana ili kuhakikisha watu zaidi wanaokolewa," alisema Balozi Nchimbi.

***Imeandaliwa na Elizabeh Zaya na Thobias Mwanakatwe**



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA (AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. 2760042 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

ANDREW YONA KITUA .................... ACCUSED PERSON

To:
Andrew Yona Kitua
Mapinga Area, Bagamoyo Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 21 day of November 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 22 day of October 2024

RESIDENT MAGISTRATE

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution


Served Upon Me/us:

Name ....................

Signature ....................

Qualification/Relationship

Date ....................



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI

KISUTU - DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI NO. 26490 YA 2024

CONTRACTORS REGISTRATION BOARD ..... MDAI

DHIDI YA

RAHKY ENGINEERING & INFRASTRUCTURE LTD AND 3 OTHERS ..... MDAIWA

KWA: 1. RAHKY ENGINEERING & INFRASTRUCTURE LTD
2. AYUBU HUBERT BAHATI
3. FRANKLIN PETER LAWO.
4. ATHANAS LAWO.

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya Mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 06/12/2024 Saa 9:00 ASUBUHI Kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutajwa shauri hilo ni lazima mlete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIA:**
Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea Kuitwa Shaurini, itaweza kusikiliza bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 08 Mwezi wa 11, 2024

HAKIMU MKAZI
KISUTU - DAR ES SALAAM

*Kwa Maoni kuhusu habari hii: Piga simu / SMS / WhatsApp : +255 677 020 701. Email: customerrelations@guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

UCHAGUZI WA MITAA

# CCM, CHADEMA 'weka, tuweke' miji ya kimkakati

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

ZIKIWA zimebaki siku nane kabla ya kufanyika kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, takwimu za awali kuhusu namna vyama vilivyosimamisha wagombea, zinaonesha kutakuwa na mchuano mkali kati ya CCM na CHADEMA katika miji inayotajwa kuwa ya kimkakati kisiasa.

Jijini Dodoma juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa alitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa mchakato wa uchaguzi huo, ikionesha kuwa vyama vya upinzani vikiongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) vilijikita zaidi katika maeneo ya miji ya kimkakati kisiasa kusimamisha wagombea.

Ni mkakati unaolenga kujiimarisha kisiasa katika miji na majiji husika kuelekea Uchaguzi Mkuu mwakani, huku kukiwa na kumbukumbu ya CHADEMA kufanya vizuri katika miji hiyo wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, ikishinda viti vya ubunge katika majimbo kama vile Mbeya Mjini, Musoma Mjini, Tarime Mjini, Bukoba Mjini, Arusha Mjini, Moshi Mjini, Ubungo, Kibamba na Ukonga.

Katika ufafanuzi wake, Waziri Mchengerwa alisema kuwa kati ya nafasi 80,430 zinazogombewa, vyama 18 vya siasa vimeweka wagombea katika nafasi 30,977 sawa na asilimia 38.51, ukiacha Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho imeweka wagombea katika nafasi zote.

Kati yake, nafasi za mwenyekiti wa kijiji zinazogombewa ni 12,280, upinzani ukiweka wagombea katika nafasi 6,060 sawa na asilimia 49.35 ya nafasi hizo; mwenyekiti wa mtaa kuna nafasi 4,264 lakini upinzani umweka wagombea katika nafasi 3,281 sawa na asilimia 76.94 ya nafasi hizo.

Nafasi za mwenyekiti wa kitongoji zinazogombewa ni 63,886, lakini vyama 18 vya siasa vimeweka wagombea katika nafasi 21,636 sawa na asilimia 33.87 ya nafasi hizo.

**MIJI YA KIMKAKATI**

Waziri Mchengerwa alieleza namna mchuano ulivyo katika kusimamisha wagombea maeneo ya miji, akiweka wazi kuwa "huko ndiko kwenye maeneo ya kimkakati kisiasa".

Alisema Jiji la Mbeya lina mitaa 181, CCM walichukua fomu kwenye mitaa yote 181, CHADEMA walichukua fomu katika mitaa 154 na wameteuliwa kwenye mitaa 153; CUF walichukua fomu katika mitaa 154 na wameteuliwa wote, ACT Wazalendo walichukua fomu katika mitaa tisa na wameteuliwa wote, TLP walichukua fomu katika mtaa mmoja na mgombea wao huyo ameteuliwa.

Katika Jiji la Arusha, Waziri Mchengerwa alisema kuna mitaa 154, CCM walichukua fomu katika mitaa yote 154, lakini wagombea wao tisa hawakuteuliwa, waliwekewa pingamizi. CHADEMA walichukua fomu katika mitaa 154, waliorejesha ni 142 na walioteuliwa ni 95.

Alisema Jiji la Dodoma lina mitaa 222, CCM walichukua fomu kwa mitaa yote 222, CHADEMA walichukua fomu kuwania mitaa 81 na wameteuliwa 67.

Mchengerwa alisema kuwa katika Jiji la Mwanza, CCM walichukua fomu kuwania mitaa yote 175, CHADEMA walichukua fomu kuwania mitaa 160 na wameteuliwa 153.

Waziri huyo alisema kuwa Manispaa ya Temeke ina mitaa 142, CCM walichukua fomu kuwania mitaa yote 142. CHADEMA walichukua fomu kuwania mitaa 105, wameteuliwa 96.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi yenye mitaa 60, CCM walichukua fomu za mitaa yote, CHADEMA walichukua fomu za mitaa 59 na wameteuliwa 46, CUF walichukua fomu mitaa miwili na wameteuliwa wote, ACT walichukua fomu 22 na wameteuliwa 16.

Alisema kuwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida yenye mitaa 53, vijiji 19 na vitongoji 83. Katika maeneo hayo CCM walichukua fomu kuwania mitaa, vijiji na vitongoji vyote. CHADEMA walichukua fomu kuwania mitaa 23, vijiji sita na vitongoji 25 na wameteuliwa katika mitaa ni 19, vijiji sita na vitongoji 23.

Waziri Mchengerwa alisema kuwa katika Manispaa ya Iringa yenye mitaa 131, CCM walichukua fomu kwenye mitaa yote, CHADEMA walichukua fomu kuwania mitaa yote 131 na wameteuliwa 127.

Alisema Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ina mitaa 67, CCM walichukua fomu kwa mitaa yote, CHADEMA walichukua za mitaa 42 na wameteuliwa 40.

Alisema katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ambayo ina mitaa 171, CCM walichukua fomu kwa mitaa yote, CHADEMA walichukua fomu katika mitaa 133 na wameteuliwa 132.

Halmashauri ya Mji wa Tarime ina mitaa 81, CCM walichukua fomu kwa mitaa yote, CHADEMA walichukua fomu za kuwani mitaa 79 na wameteuliwa 76.

Mjini Bunda kuna mitaa 84, CCM walichukua fomu kwa mitaa yote, CHADEMA walichukua za mitaa 73 na wameteuliwa 70.

Katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu yenye mitaa 58, CCM walichukua fomu kwenye mitaa yote, CHADEMA walichukua 39 na wameteuliwa.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ina vijiji 101, CCM walichukua fomu kuwania vijiji vyote, CHADEMA walichukua fomu kutaka kuongozi vijiji 71 na wameteuliwa 67.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ina vijiji 76, CCM walichukua fomu katika vijiji vyote, CHADEMA walichukua vijiji 76 na wakateuliwa 73, ACT walichukua vijiji 17 na wakateuliwa 17.

Pia alisema kuna vitongoji 513 ambapo CCM walichukua katika vitongoji vyote na kuteuliwa wote, CHADEMA walichukua 449 na wakateuliwa 443, ACT walichukua 11 na wameteuliwa 10.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Musoma Vijijini ina vijiji 88 na vitongoji 500. CCM walichukua fomu kwa vijiji na vitongoji vyote, huku CHADEMA wakichukua fomu katika vijiji 81 na wakateuliwa 78 na vitongoji 397 na wameteuliwa 359.

Hata hivyo, Waziri Mchengerwa alibainisha kuwa takwimu hizo ni kabla ya kukamilika kwa hatua ya rufani za uteuzi, hivyo takwimu sahihi za walioteuliwa zitatolewa baadaye.

***Kwa Maoni kuhusu habari hii: Piga simu / SMS / WhatsApp : +255 677 020 701. Email:customerrelations@guardian.co.tz***

# Makonda afunguka shambulio la Tundu Lissu, uvamizi studio

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

HATIMAYE Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amevunja ukimya kuhusu tuhuma zilizoibuliwa dhidi yake na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akimtaja hadharani kwamba ndiye kiongozi wa umma aliyeongoza kikosi cha wasiojulikana waliomshambulia kwa nia ya kumuua miaka saba iliyopita.

Makonda kwa mara ya kwanza alitoa ufafanuzi hadharani jana, akijibu tuhuma hizo, huku akihoji Lissu ana uhakika gani kuwa shambulio hilo aliliongoza.

Ni wakati akiwajibu waandishi wa habari waliomwuliza maswali wakati wa utoaji ripoti ya miezi sita ya uongozi wake, hafla iliyohudhuriwa na watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini na kurushwa moja kwa moja na vituo vya televisheni vya kitaifa.

Makonda alisema amemshangaa Lissu kwa nini hadi jana alikuwa hajaenda mahakamani kwa kuwa ni zaidi ya miaka saba sasa tangu shambulio hilo kutokea (Septemba 2017).

"Lissu anavyonituhumu kuwa mimi nilihusika kumpiga risasi, si (tuhuma) za kweli hata kidogo, badala yake anatafuta huruma kwa wengine, yaani mimi Makonda hata mgambo sijaenda, ninaanzaje kufanya haya na sipendi kuhangaika kumjibu Lissu na mjue hakuna Rais anayeweza kuunda kikosi na kutenda mambo yasiyofaa, hakuna," alisema.

Makonda pia alizungumzia kwa mara ya kwanza hadharani tuhuma za kuvamia studio za Clouds Media, akisema anawashangaa waandishi wa habari hadi jana walikuwa hawajawahi kumhoji Dk. Harrison Mwakyembe kuhusu kilichomo katika ripoti yake ya uchunguzi wa tukio hilo.

Alisisitiza kuwa akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alikuwa na urafiki mkubwa na wamiliki na wafanyakazi wa chombo hicho cha habari, hata kuwanunulia magari na baadhi ya vifaa vya kazi, hivyo tuhuma dhidi yake kuvamia studio zao si za kweli.

Kuhusu utendaji kazi ndani ya miezi sita mkoani Arusha, Makonda alisema kuwa katika sekta ya utalii, mapato yameongezeka na kufika trilioni 2.7 huku magari ya utalii baada ya filamu ya Tanzania The Royal Tour yakiongezeka, yakiwamo yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufikia Sh. bilioni 336 tangu Rais Samia alipoingia madarakani.

Alisema hospitali nne mpya za wilaya zimejengwa na tatu kukarabatiwa huku idadi ya watoa huduma za afya ikiongezwa ili kuondoa changamoto kwa wananchi kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya huku vifo vya kinamama vikipungua sambamba na vya watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Alisema wameimarisha pia huduma za maji, ulinzi na usalama na kwamba Desemba Mosi mwaka huu, Rais Samia Hassan Suluhu anatarajia kukutana na viongozi wa kimila jamii ya Wamasai na viongozi wengine muhimu ili kujadili mustakabali wa wananchi wanaoishi wilayani Ngorongoro na kutoa majibu sahihi.

Akizungumzia kuhusu kuenguliwa kwake kwa nafasi ya Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Makonda alisema, "Nilipoenguliwa kutoka Katibu Siasa na Uenezi Taifa ulikuwa ni usiku mkubwa na wenye mawazo kuwa nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha nitafanyaje, sababu nilianza kusahau, lakini nilipofika Arusha, nimekutana na watu wakarimu, wenye bidiii za kufanya kazi na kutafuta fedha."


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SAMWEL KAPULWA KOTIPWE | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO - DAKAWA, MVOMERO | J&J RECOVERIES | 30/11/2024 |
| 2 | RASHID ATHUMAN MGAYA | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI- DAKAWA, MVOMERO | J&J RECOVERIES | 30/11/2024 |
| 3 | STEVEN BIYARA MSANO | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO-MVUMI, KILOSA | J&J RECOVERIES | 30/11/2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.



Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Cyprian Luhemeja, akionesha vitabu vya mazingira vilivyoandikwa na mtoto wa kitanzania Georgina Magesa wakati akizungumza na Watanzania wanaoshiriki Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) unaofanyika katika Mji wa Baku, Azerbaijan jana. **PICHA: ROBERT HOKORORO**

UCHAGUZI WA MITAA...

# ACT kutinga mahakamani kupinga wagombea kukatwa

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimezindua Ilani ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji ya 2024-2029, kikitangaza kitafungua kesi mahakamani kupinga wagombea wake kuenguliwa katika uchaguzi huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ilani hiyo kwenye ofisi za Makao Makuu ya chama hicho mkoani Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti Tanzania Bara, Isihaka Mchinjita, alisema wameamua kwenda mahakamani ili kusaka alichokiita "haki ya wanachama walioenguliwa".

Mchinjita alisema kuwa licha ya baadhi ya wagombea wa chama hicho kuenguliwa kutokana na sababu mbalimbali ambazo hawakubaliani nazo, wataendelea kushiriki katika mchakato wote wa uchaguzi huo uliopangwa kufanyika tarehe 27 mwezi huu.

"Sisi (ACT) ndiyo tulifungua kesi mahakamani kupinga wagombea kupita bila kupingwa. Sisi pia tulikwenda mahakamani kupinga TAMISEMI kusimamia uchaguzi, kukawa na kesi nyingine ya aina hiyo, tutashindwa kuendelea na kesi yetu lakini tuliungana na waliotangulia kufungua kesi.

"Isivyo bahati, mahakama ilibariki TAMISEMI iendelee kusimamia mchakato wa uchaguzi huu. Kinachotokea sasa kuengua wagombea wa upinzani, ndicho kile ambacho tulikipinga tangu awali.

"Wanaosikiliza rufani, hao maDAS (katibu tawala wa wilaya), wengi wao ni makada wa CCM. Tutashiriki uchaguzi huu hadi mwisho. Mapambano yanaendelea.

"Tumeona tunapaswa kwenda mahakamani kupinga kuenguliwa wagombea wetu. Wameenguliwa kinyume cha kanuni. Tunakwenda mahakamani ili wananchi wapate haki ya kuchagua nani anapaswa kuwa kiongozi wao," alisema.

**UZINDUZI ILANI**

Kiongozi wa ACT Wazalendo, Dorothy Semu, akizindua ilani hiyo, alianza kwa kutoa pole kwa wananchi kutokana na tukio la kuporomoka kwa jengo la ghorofa huko Kariakoo, jijini Dar es Salaam, kisha akasisitiza kuwa chama hicho kimechoshwa na alichokiita "uporaji wa demokrasia na kupuuza sauti na madai ya wananchi".

Alisema chama chao kimechoshwa na ubadhirifu na uongozi usiowajibika, huduma mbovu za kijamii, uchakavu wa miundombinu mijini, ubovu wa miundombinu vijijini na uchumi usiotengeneza ajira na usioleta maendeleo vijijini.

"Kwa miaka mitano tumelazimika kuishi pasipo kuwa na uwakilishi wa kweli; tumekuwa na viongozi wasiochaguliwa na kuwajibika kwa wananchi katika ngazi za serikali za mitaa, vijiji na vitongoji.

"Matokeo yake, serikali za mitaa kuanzia halmashauri za vijiji, wilaya, miji na majiji vimedumaa; wananchi wamepoteza sauti zao za uamuzi; vyombo vyao vya kufanya uamuzi vimedorora," alisema.

Dorothy alisema kuwa upatikanaji huduma za msingi kama vile maji, barabara, usafi wa mazingira, elimu, umeme na huduma zingine ni changamoto kubwa, akidokeza kuwa wastani wa kaya 29 kati ya 100 ndio zanapata huduma ya maji safi na salama vijijini.

"Nchini kote hakuna umeme wa uhakika, huku hali vijijini ni tete zaidi, kwani kaya zilizounganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa vijijini ni asilimia 11 tu. Hali ya usafi wa mazingira ni mbaya, huduma za uzoaji taka ni duni na miundombinu ya maji taka ni chakavu.

"Hali za wananchi ni duni na ziko katika hatari kubwa sana. Watanzania milioni 16, wananchi chini ya mstari wa umaskini uliokithiri. Kati yao, zaidi ya milioni nane wanaishi katika umaskini wa kutupwa na asilimia 81 (watu milioni 12.9) ya watu masikini nchini wanaishi vijijini, huku kasi ya kupunguza umasikini vijijini ni ndogo sana," Dorothy alitamka kwa hisia kali.

Alisema ilani yao aliyoizindua jana, ni agano la uongozi unaowajibika na tamko lao dhidi ya rushwa, uzembe na ubadhirifu na ni dira yao katika kutoa huduma bora za jamii vijijini na mijini; kuimarisha na kuboresha miundombinu, kukuza uchumi, ajira na kuondoa umasikini.

Wakili kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Maduhu William, aliyehudhuria hafla ya uzinduzi wa ilani hiyo, alisema amefurahishwa na hatua hiyo ya ACT kuwa na ilani ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kuwa vyama vingi vinajikita katika ilani ya Uchaguzi Mkuu pekee.

Alisema fasili ya nne ya ilani hiyo imemkosha zaidi kutokana na kuweka msisitizo katika ulinzi wa maisha ya watu, hivyo wagombea wakatilie makazo kuimarisha ulinzi huo na kukomesha mauaji ya watoto, wanawake, vikongwe na wenye ulemavu nchini.

ACT-Wazalendo kimekuwa chama cha kwanza nchini kuwa na Ilani ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

***Kwa Maoni kuhusu habari hii: Piga simu / SMS / WhatsApp : +255 677 020 701. Email:customerrelations@guardian.co.tz***

# UTT AMIS yajivunia thamani ya mifuko kuongezeka hadi tril. 2.2/-

**Na Frank Monyo**

MKURUGENZI Mtendaji wa UTT AMIS, Simon Migangala, amesema juhudi za kuboresha mifumo ya kidijitali, mazingira thabiti ya uwekezaji na utulivu wa soko, zimewezesha taasisi hiyo kupata mafanikio makubwa, thamani ya mifuko ikiongezeka hadi Sh. trilioni 2.2 kufikia Juni 30 mwaka huu kutoka Sh. trilioni 1.6 Juni 2023.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa Mkutano Mkuu wa 16 wa Mfuko wa Umoja uliokutanisha wawekezaji wa mifuko ya taasisi hiyo ambayo ni Umoja Fund, Wekeza Maisha Fund, Watoto Fund, Jikimu Fund, Liquid Fund na Bond Fund.

"Mifuko yetu imefanya vizuri sana, ikikua kutoka Sh. trilioni 1.6 mwaka 2022/23 hadi Sh. trilioni 2.2 mwaka 2023/24, ikiwa na faida ya asilimia 12 au zaidi kwenye kila mfuko, kwa mujibu wa mpango huo wa uwekezaji wa pamoja.

"Tunawashukuru wawekezaji wetu kwa imani yao endelevu, pamoja na serikali. Tumejizatiti kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini. Tunatarajia mafanikio makubwa zaidi," alisema Migangala.

Alisisitiza kuwa mkakati wa sasa wa UTT AMIS ni kuboresha miundombinu ya teknolojia ili kufikia watanzania wengi zaidi.

Aliongeza kuwa faida ya mwaka 2023/24 ni zaidi ya Sh. bilioni 250, akiitaja ni ongezeko kubwa kulinganishwa na mwaka uliopita.

Mkurugenzi huyo alisema mpango huo wa uwekezaji wa pamoja umeweka lengo la kuongeza thamani ya mifuko hadi Sh. trilioni 2.5 ifikapo mwaka ujao wa fedha, akidokeza kuwa tayari wameona dalili za kufikiwa kwa lengo hilo kwa hesabu za miezi minne ya mwanzo kufikia mwezi Oktoba mwaka huu.

Alisema licha ya changamoto za kimataifa kama vile vita na taharuki ya kisiasa, uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika, ukirekodi ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023 na matarajio ya ukuaji wa asilimia 5.4 mwaka huu (2024).

Mkurugenzi huyo alisema mfumuko wa bei ulibaki katika kiwango cha asilimia 3.1 chini ya matarajio ya asilimia 5.0. Ukuaji wa sekta ya mitaji pia ulionekana; bei za hisa ziliongezeka kwa asilimia 9.3 katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Migangala alikiri kuwa idadi ya watanzania wanaowekeza katika mifuko hiyo ni ndogo, kauli iliyoungwa mkono na Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS, Prof. Faustine Kamuzora, aliyesema, "licha ya mifuko ya uwekezaji kuwa na faida nyingi, kumekuwapo mwitikio mdogo wa wananchi kujiunga kutokana na kukosa elimu ya uwekezaji".

Aliongeza kuwa wakati watanzania wakiwa zaidi ya milioni 60 (Sensa ya Watu na Makazi 2022), waliowekeza katika mifuko hiyo hawazidi milioni moja, hivyo elimu zaidi inahitajika ili kufahamu umuhimu wake.

"Wananchi katika hili wanapaswa kujua kwamba usipokuwa na uwezo wa kutengeneza fedha wakati umelala, ni hatari kwako na badala yake ni lazima kila siku ukimbizane na biashara na kila senti unayoipata na wakati mwingine mambo yanaweza yasiwe mazuri kwako katika kukimbizana huko.

"Hivyo, unavyowekeza fedha katika mifuko kama hiyo, mtaji wako unaendeshwa na wataalamu ambao wanajua soko linavyokwenda na kukuzalishia faida kila uchwao," alisema.

Aliongeza kuwa katika kukabiliana na changamoto hiyo, UTT AMIS inatekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza ujumuishi wa kifedha na kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

"Mwaka huu umekuwa wa mafanikio makubwa kwa mifuko yetu kutokana na imani kwa wataalamu wetu. Mifuko ni salama na hatari zinazohusiana na uwekezaji ni ndogo. Watanzania wanaweza kuwa na uhakika wa kupata faida mwishoni mwa mwaka," alisema Prof. Kamuzora.

# TANGAZO

# INLAND DEVELOPMENT TANZANIA

**DIOCESE OF TABORA**
**P.O. BOX 1286**
**TABORA, Tanzania, E.A**

**Office Tel. +255 763 274 165**
**+255 758 852 195**
**Email- idtprocurement@gmail.com**

## PRE- QUALIFICATION OF SUPPLIERS FOR PROVISION OF GOODS AND SERVICES NOTICE FOR THE YEAR 2024/2025

## IDT

## TENDER NUMBER 01/FY2024-25/0001

**Background**
**INLAND DEVELOPMENT TANZANIA (IDT)** is a Non - Governmental Organization legally registered under the Act NO. 24 of 2002 on August 2019 with registration **NO. 00NGO/R/0489** to operate in Tanzania Mainland. Inland Development Tanzania (IDT) is the inheritor name of African Inland Church Tanzania (AICT), which was a Faith Based Organization (FBO) and non-profit organization. The organization's head office is located in Tabora Municipal at AICT Diocese of Tabora, opposite the Kitete Primary School. IDT is currently implementing programs in the Tabora region and has sub-offices in each council of the Tabora region. IDT aims to develop endeavors and empower the community to overcome poverty, Ignorance, and diseases and advocate for human rights.

IDT invites application from eligible, competent and qualified vendors and service providers to apply for Prequalification for provision of Car hiring services.

| S/N | Description of the Service |
|---|---|
| 1 | Provision of Transport car hire services. |

**QUALIFICATION REQUIREMENTS**

Interested suppliers are advised to include the following in their applications;

i. Brief overview of the company and key staff (Company Profile) including physical business address.
ii. Latest Business Registration Certificate or Certificate of Incorporation
iii. Copy of TIN and VAT registration certificates and valid tax Clearence (Tax Compliance Certificate) in Tanzania
iv. Written endorsement of at least three reputable customers dealt with for the past 2 years other than IDT.
v. Valid Business licenses
vi. Current Audited financial statement for two consecutive years i.e. 2022 and 2023 (signed and stamped).
vii. Payment terms 100% after delivery
viii. Evidence of two LPO/Contracts of similar assignments for the last three years, and at least two (2) names and addresses of clients served.

**ELIGIBILTY**

To be considered for the award, vendors must currently be legally operating in Tanzania, and the quotation must include all of the following information:

- Ability to meet or exceed the requirements/technical specifications outlined in the TOR
- Ability to deliver the items/services specified.
- Ability to meet timeline as per the flexibility required.

**Evaluation Criteria:**

- Competitive Pricing.
- Financial capability.
- Company Experience.
- References and feedback from previous clients.

**Note**

1. All quotes must be in Tanzanian Shillings and enclosed in a plain sealed envelope.
2. Late or incomplete bids will not be accepted.
3. Electronic bids will not be accepted.
4. The language of bid submission is English.
5. IDT may cancel the solicitation and not award.
6. Issuance of requests for quotes does not constitute a contractual commitment by IDT.
7. IDT reserves the right to disqualify any offer based on the offeror's failure to follow the solicitation instructions.
8. IDT reserves the right to waive minor proposal deficiencies that can be corrected before award determination to promote competition.
9. IDT will contact all offerors to confirm the contact person, address, and the proposal submitted for this solicitation.
10. IDT will not compensate Vendors for their response to the solicitation.
11. IDT may choose to award only part of the scope of work in the solicitation or to issue multiple awards for the scope of work.
12. Information pertaining to and obtained from the Vendor as a result of participation in this solicitation is confidential. The Vendor consents to the disclosure of the documents submitted by the Vendor to the reviewers involved in the selection process. Please note that non-disclosure agreements bind all reviewers.

The deadline for the submission of proposals is 1100hrs East Africa Time on **01st November 2024.**

Question and clarification are due on **31th October 2024 at 0400hrs** East Africa Time through Email: at **idtprocurement@gmail.com** with the subject line "Request for Clarification:

**Interested, eligible dealers/vendors should deliver physically their Proposal/quotation to,**

**The Procurement Committee,**
**INLAND DEVELOPMENT TANZANIA**
**P.O. box 1286**
**Tabora**

IDT will open all bids on **01st November 2024 at 1205hrs** in the presence of the bidder's representatives who choose to attend. The present Bidders' representatives shall sign a register evidencing their attendance.

**The terms of reference (TOR) for more details can also be accessed through (www.)**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA FEDHA

## MWALIKO WA KUSHIRIKI MKUTANO WA PILI WA JUMUIYA YA WAHASIBU WAKUU WA SERIKALI AFRIKA-AAAG

Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Wahasibu wa Serikali wa Afrika mwaka 2024 (AAAG) utakaofanyika jijini Arusha kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba, 2024.

Mkutano wa pili wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Serikali Afrika utakuwa na mada mtambuka ambazo zitasaidia watumishi wa kada mbalimbali kuwaongezea ujuzi na Maarifa.

Pia Mkutano huu utasaidia Viongozi na Watumishi wa Tanzania kupata nafasi ya kubadilishana uzoefu na kupeana fursa na Viongozi na Watumishi toka nchi nyingine za Afrika, Benki ya Dunia na IMF. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ada ya ushiriki ya mkutano ni **Shilingi za Kitanzania 1,300,000/=** kwa kila mshiriki. Hivyo, Mamlaka husika zinaombwa kuwaruhusu na kuwalipia Wahasibu, Wakaguzi wa Ndani, Maafisa Usimamizi wa Fedha, Maafisa TEHAMA na watumishi wa kada nyingine kuhudhuria mkutano huu.

Washiriki wote wanatakiwa kuanza kijisajili kupitia lango (portal) lifuatalo: https://conference.aaag.org.zm kuanzia sasa hadi tarehe 01 Disemba, 2024 na ada ya ushiriki ilipwe kupitia **akaunti namba 9924915301 yenye jina African Association of Accountants General (AAAG).**

Aidha, kwa Taasisi za Umma, Kampuni mbalimbali na watu binafsi wanaotaka kudhamini Mkutano huu kwa lengo la kujitangaza kibiashara na kufanikisha Mkutano huu; Wizara ya Fedha inawakaribisha.

Kwa mawasiliano zaidi piga Namba ya simu +255 713 525 592 barua pepe, veronica.kishala@hazina.go.tz na evans.sayile@hazina.go.tz Sanduku la Posta ni Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha S.L.P 2802, Dodoma.

Pia kama muombaji amesahau namba ya simu, barua pepe na Sanduku la Posta anaweza kupata mawasiliano kupitia wakuu wa Hazina Ndogo waliopo kila mkoa Tanzania bara na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Zanzibar.

**Kwa Nakala Ngumu tafadhali wasilisha kwa anuani ifuatayo:**

**Sekretariati ya Kamati ya Maandalizi Mkutano wa AAAG,**
**Wizara ya Fedha**
**Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**
**Jengo la Hazina (Ghorofa ya Pili),**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete,**
**S.L.P 2802,**
**DODOMA.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

**KATIBU MKUU - HAZINA**
**Novemba, 2024**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji Taifa Stars AFCON 2025 inawahusu, pambaneni

**USHINDI** wowote ule unatakiwa kwa Timu ya Taifa ya Tanzania ili kuweza kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika, zitakazopigwa mwakani nchini Morocco.

Yalikuwa ni mabao ya Simon Msuva na Feisal Salum yaliyoipa ushindi wa 2-0 dhidi ya Timu ya Taifa ya Ethiopia, iliyokuwa ikichezea mechi yake nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ukichezwa Uwanja wa Des Martyrs jijini Kinshasa juzi.

Ushindi huo unaifanya Stars kufikisha pointi saba kwenye Kundi H, ikiendelea kushika nafasi ya tatu, nyuma ya Guinea iliyo nafasi ya pili kwa pointi tisa baada ya juzi kushinda bao 1-0 nyumbani dhidi ya vinara wa kundi hilo, DR Congo.

Wakongomani wameshafuzu, Ethiopia haina matumaini ya kufuzu tena, hivyo nafasi moja iliyobaki inapiganiwa na Tanzania pamoja na Guinea.

Kwa bahati nzuri timu hizo zitamalizana kesho Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, na mshindi ataungana na DR Congo kwenda Morocco hapo mwakani.

Sare yoyote haiisaidia Tanzania, kwani Guinea itakuwa imefuzu, hivyo wakati ni sasa kwa Watanzania kuungana kwa pamoja kuhakikisha wanaiunga mkono Taifa Stars itakaposhuka dimbani kesho ili kuweza kushinda mechi hiyo.

Ijulikane wazi kufuzu kwa AFCON hii kutaisaidia mno Tanzania kwenda kupata uzoefu kwani baada ya hapo itakuwa mwenyeji wa fainali za msimu wa 2027 kwa ushirikiano wa nchi za Kenya na Uganda.

Itakuwa ni aibu na haitopendeza kwa nchi yetu kushindwa kufuzu AFCON ya mwakani na kusubiri kucheza fainali hizo kwa uenyeji 2027.

Huu ni wakati kwa wachezaji wa Taifa Stars kuionesha Afrika kuwa nchi hii kwa sasa ni moja kati ya zile zinazokuja juu kwa kasi na ndiyo maana ligi yake ni ya sita kwa ubora Afrika.

Wachezaji wanatakiwa kutoa machozi, jasho na damu hata ili kuipigania nembo na bendera ya timu ya taifa kwani watakaopambana na kutinga AFCON watahesabika kama mashujaa wa nchi kwa upande wa soka. Kwa upande wa viongozi wa serikali, Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), na wadau wengine ni wakati wa kuipigani Taifa Stars, lakini kimya kimya hasa kutokana na rekodi yake isiyovutia katika kipindi cha hivi karibuni hasa inapocheza nyumbani hasa katika hatua kama hizi.

Rekodi haziibebi Taifa Stars hasa linapokuja suala la mechi za maamuzi hasa ikiwa nyumbani, lakini kwa kuwa rekodi zipo kwa ajili ya kuvunjwa, tunaamini wachezaji watajituma mwanzo mwisho katika kufanikisha lengo hilo la kufuzu ACON 2025.

Ikumbukwe pia kila inapofanyika hamasa, ndiyo Taifa Stars hupoteza kwa namna ya kushangaza, jambo ambalo hatutaki kuona kipindi hiki likitokea.


Hivyo hiki ni kipindi ambacho wachezaji wetu wanapaswa kupewe huduma nzuri za kambi, posho na kila kitu, lakini kila mwenye zawadi au ahadi yoyote asubiri kwanza mpaka mechi imalizike, tutakaposhinda ndipo sasa iruhusiwa kila mmoja kuwazawadia, jambo ambalo tunaamini likifanyika kabla litawaongezea presha uwanjani.

Kwa sasa waachiwe makocha, wakiongozwa na Kocha Mkuu, Hemed Suleiman 'Morocco' wafanye kazi yao ya kiufundi na wachezaji wayashike hayo tu, si kufikiria tena wakishinda wanapata kiasi gani cha pesa.

Vile vikundi vya hamasa vinatakiwa tu kwenda uwanjani na kushangilia kwa nguvu zote mwanzo mwisho, na si kupita huku na kule kabla ya mechi na kuwatia presha wachezaji.

Tunaamini kwa Stars hii ya sasa inaweza kabisa kuifunga Guinea na kutinga fainali hizo za AFCON kama kila mmoja atatimiza wajibu wake uwanjani na mashabiki kama mchezaji wa 12 watatekeleza wajibu wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Machawa' wamemfukuzisha kazi Kocha Gamondi Yanga

Na Adam Fungamwango

**SIDHANI** kama kuna mwanachama na shabiki wa Yanga asiyejua kwamba aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi alikuwa kocha bora.

Hakuna asiyejua kuwa alikuwa ni kocha mzuri kiufundi uwanjani kiasi cha kuwapa kazi makocha wote Tanzania jinsi gani ya kumkabili ukienda kucheza naye.

Kwanza kabisa alikuwa anahitaji wachezaji wenye fiziki ya hali ya juu. Ndiyo maana Yanga akawa na timu yenye wachezaji wenye fiziki ya hali ya juu kuliko wachezaji wa timu nyingine.

Akafundisha soka la kasi, kukimbia muda wote na kuhaha uwanjani kama mbwa mwenye njaa anayekimbiza swala. Hakutaka mchezaji yeyote kuwa abiria uwanjani. Timu ilikuwa inakabia juu. Makipa na mabeki wa timu pinzani wanapoanza mpira wanakutana na shinikizo kutoka kwa mastraika ambao kazi yao namba moja ni kufunga, lakini ya pili ni kuhakikisha mabeki na kipa wa timu pinzani hawaanzi mpira wakiwa huru. Mfumo huu uliwapa tabu sana wapinzani.

Akaondoka kwenye soka la kumtegemea mtu mmoja, Fiston Mayele, badala yake akatengeneza mfumo wa wachezaji wote kuwa wafungaji. Kabla ya hapo Yanga ilijengwa kwa kumzunguka Fiston Mayele wakati wa Kocha Nasreddine Nabi.

Wachezaji wa Yanga wakagawana mabao, wafungaji wakawa kina Pacome Zouzoua, Stephane Aziz Ki, Maxi Nzengeli ambao ni viungo washambuliaji, hata Mudathir Yahaya ambaye ni kiungo mkabaji, akainukia kuwa mfungaji hodari wa timu hiyo.

Timu ikaogopeka si nchini tu hata na nje ya nchi, kiasi cha Yanga kuingia kwenye moja ya timu tishio barani Afrika kutoka Tanzania baada ya watani wao wa jadi, Simba.

Haya yote yaliletwa na Gamondi, raia wa Argentina, ambaye ufundishaji wake uliwakuna viongozi wa klabu mbalimbali barani Afrika.

Kwa namna ya kushangaza kocha huyo amefukuzwa. Mpaka sasa hakuna maelezo kutoka kwa viongozi wa Yanga sababu za kufanya hivyo. Pamoja na hayo kila mmoja anajua kuwa Yanga ilipoteza mechi mbili mfululizo dhidi ya Azam FC ilipofungwa bao 1-0, na ikachabangwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United.

Binafsi, sioni mantiki yoyote ya kocha kama Gamondi kutimuliwa baada ya kufungwa mechi mbili mfululizo kwani ukizitafuta sababu zinajulikana.

Mechi ya kwanza Yanga iliathirika na kadi nyekundu ya Ibrahim Hamad 'Bacca', na mechi ya pili ilimkosa mchezaji huyo pamoja na Dickson Job aliyekuwa na kadi nyekundu, pamoja na Yao Kouassi.

Hizi ni sababu tosha ambazo zilikuwa zinamwondoa Gamondi kwenye lawama, ingawa ukweli lazima usemwe kuwa tangu kuanza kwa msimu huu Yanga haipo kwenye kiwango kile kilichozoeleka.

Hata hivyo, bado sababu si za Gamondi. Ndani ya Klabu ya Yanga kuna wapambe ambao siku hizi wanajulikana kama 'chawa.'

Hawa watu wamekuwa na uswahiba mkubwa na viongozi. Hawa ndiyo sumu ndani ya klabu kiasi cha kusababisha kocha huyo bora kabisa kutimuliwa.

Mchana wanakaa na viongozi, lakini usiku unakutana nao wako na wachezaji kwenye kumbi za starehe mpaka alfajiri.

Machawa hawawaambii ukweli viongozi wala wachezaji, wanabaki kuwasifia tu. Kundi hili ni hatari zaidi, linajua kuunganisha watu na kisha kukaa pembeni wanasubiri anguko ili kisha wauwashe moto.

Hao hao badala ya kuwaambia viongozi wao kuwa wachezaji wameshuka viwango kwa sababu ya starehe, wanakwenda kumkaanga kocha ili aonekane mbaya kwa sababu wachezaji wana manufaa nao.

Uongozi wa klabu lazima uwatazame machawa hawa kwa jicho la ukali kwani wanaweza kuwaharibia timu.

Wachezaji wa Yanga ambao wanajiona wamekuwa wakubwa na mastaa, wanatakiwa kutambua ligi ni ngumu msimu huu na timu zinazotaka ubingwa zimeongezeka, watani zao, Simba wamebadilika, wamefanya usajili mkubwa na kiufupi kila timu imejipanga kwa hesabu zake, hivyo haitakuwa rahisi kwao kutetea ubingwa endapo wataendelea kujiona kama wao ndio bora kuliko wengine na kuendekeza starehe zilizosababisha viwango vyao kushuka na mzigo wote kumwangukia Gamondi.

## NMB yakabidhi vifaa shuleni, vituo vya afya

**Na Mwandishi Wetu,**

KATIKA kuhakikisha inaendelea kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha huduma za jamii kwa wananchi wake katika sekta za elimu na afya, Benki ya NMB imetoa vifaa mbalimbali katika shule za msingi, sekondari na zahanati za mikoa ya Morogoro na Mtwara.

Vifaa hivyo ambavyo vimegharimu Sh. milioni 56.7 ni pamoja na madawati 219 kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi za Mafisa 'A' iliyoko Manispaa ya Mororgoro, Shule za Msingi Njengwa na Mbemba za Halmashauri ya Mji Nanyamba, mkoani Mtwara.

Vifaa vingine ni meza pamoja na viti 220 vilivyotolewa kwa ajili ya Shule za Sekondari Kingo Manispaa ya Morogoro na Mtiniko, Mnongodi na Nyundo, zote za Halmashauri ya Mji Nanyamba, mkoani Mtwara.

Katika sekta ya afya, NMB imetoa vitanda 10 na magodoro 10 kwa ajili ya wagonjwa na vitanda maalumu viwili kwa kujifungulia, vyote vikilenga kusaidia utoaji huduma katika Hospitali ya Wilaya Nanyamba, mkoani Mtwara.

Benki hiyo pia imekabidhi magodoro 26 kwa ajili ya kuboresha huduma katika Vituo vya Afya Dinyecha na Nyundo, vyote vya Halmashauri hiyo ya Mji wa Nanyamba, mkoani Mtwara.

Akiwa mkoani Morogoro kukabidhi vifaa hivyo, Ofisa Mkuu Wateja Wakubwa na Serikali Benki ya NMB, Alfred Shao alisema sekta za afya na elimu ni maeneo ya kipaumbele kwa NMB, ambapo hutumia asilimia moja ya faida kusaidia utatuzi wa changamoto katika jamii.

"Tulipopata maombi haya ya kuchangia maendeleo ya vituo vya kutolea huduma za afya na shule katika wilaya hii, tulifarijika na kuamua mara moja kuja kushirikiana na serikali ili kuwa chachu ya maendeleo ya sekta hizo muhimu kwa jamii yetu," alisema Shao.

Meneja huyo alieleza kuwa serikali imekuwa inafanya mambo makubwa katika kuwaletea Watanzania maendeleo, ambapo NMB kama mdau mkubwa umekuwa wajibu wao katika kuunga mkono juhudi hizo za kuhakikisha huduma za kijamii zinaboreshwa zaidi.

Mkoani Mtwara, Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Olipa Hebel, alisema kuwa changamoto za afya na elimu kwa NMB ni jambo la kipaumbele kutokana na nyanja hizo kuwa msingi wa maendeleo kwa taifa.

Akizungumza kwa niaba ya Mganga Mfawidhi wa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, Katibu wa Kituo cha Afya Dinyecha, Hamisi Hassan, alishukuru benki ya NMB kwa kuwapelekea vifaa hivyo ambavyo alisema vitawasaidia kwa kuwa ni vifaa muhimu.

"Ukiviangalia ni vya kisasa na sasa mama wajawazito watajifungua kwa usalama zaidi na itatupunguzia kero ya upungufu wa vifaa tiba katika halmashauri yetu na tunawakaribisha wadau wengine waje watoe misaada," alisema Hassan. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ambaye ni Diwani wa Kitaya, Kapende Jamali Abdallah, alishukuru NMB kwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha huduma kwenye sekta hizo.

"Hadi kufikia leo ni miaka saba mfululizo benki hii imekuwa inatuunga mkono katika sekta za elimu, afya na maafa na ninaomba wasituchoke," alisema Abdallah.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23, inaonesha kuwa changamoto ya uhaba wa miundombinu na samani katika shule za msingi na sekondari nchini bado inaendelea kutishia ustawi wa elimu nchini, mikoa ya Morogoro na Mtwara ikiwa miongoni mwa yenye shule nyingi zinazokabiliwa na changamoto hiyo.



Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Mahimbo Mndolwa (kushoto), akizungumza na viongozi na waumini jana katika kilele cha sherehe za maadhimisho ya miaka 100 ya kumbukizi ya kifo cha Askofu wa Kwanza wa Dayosisi ya Zanzibar na Tanga, Hayati Frank Weston aliyefariki dunia Novemba 2, 1924, yaliyofanyika Kanisa la Anglikana Magila Msalabani, Muheza mkoani Tanga. Kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu (Kazi Maalumu), George Mkuchika aliyewavisha nishani viongozi mbalimbali wa kanisa hilo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yashauriwa kurekebisha mfumo mpya mikopo watumishi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeshauriwa kurekebisha mfumo mpya kwa watumishi kupata mikopo kidijitali bila kuweka ukomo ili kutoa fursa kwa watumishi hao bila ukomo maalumu kwa lengo la kuwaepusha na mikopo isiyo rasmi, maarufu kausha damu.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Muuguzi Wazuri Mussa (hakutaka jina la kituo chake kujulikana), aliyesema kuwa serikali kupitia Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imekuja na mfumo mpya kuwawezesha watumishi kukopa kidijitali, hatua ambayo alitaja ni nzuri.

Hata hivyo, alisema mfumo huo umewekewa kikomo cha mtumishi kukopa kiwango kuanzia Sh. 500,000 huduma inayokamilika ndani ya saa 24.

Alishauri serikali ifanyie marekebisho ili kila mtumishi anufaike na kuepukana na mikopo isiyo rasmi.

"Sisi watumishi tunaomba serikali kubadilisha kiwango ili watumishi wa ngazi zote tunufaike bila ubaguzi hasa kuelekea msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka, kiwango kipunguzwe, watumishi asilimia 80 hatuna pakwenda tumeshaanza kutapatapa tutakopa wapi?" alihoji.

Nipashe ilipozungumza kwa njia ya simu na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Juma Mkomi, alikiri kuwapo mabadiliko hayo.

Alisema kama baadhi ya watumishi hawajaridhika na mfumo huo, waandike barua kuomba kuondolewa.

"Kama wapo watumishi wanalalamikia mfumo huo mpya, waandike barua kwetu sisi tutapokea na kuifanyia kazi, si kulalamika kwenye vyombo vya habari," alisema Katibu Mkuu Mkomi kwa njia ya simu.

Novemba Mosi, mwaka huu serikali kupitia wizara hiyo ilianzisha mfumo mpya wa kidijitali kumwezesha mtumishi wake kukopa kutoka benki na taasisi za kifedha.

Mfumo huo maarufu kwa jina la ESS (Employee Self Service) unamwelekeza mtumishi wa serikali kujihudumia mwenyewe, unamwezesha kukopa muda wowote bila kwenda umbali mrefu kufuata huduma za benki au taasisi za kifedha, wala kujaza fomu yoyote.

Kupitia mfumo huo, mtumishi anamaliza kila kitu na umeziweka taasisi za fedha sehemu moja ikiwamo kunadi bidhaa zake na mtumishi anajichagulia na kusubiri fedha kupitia akaunti yake.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Prof. Janabi: Wekeza kikubwa kwenye afya ya mwili, siyo mali

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema ni muhimu jamii ikabadili mtazamo kwamba uwekezaji wa maisha ya baadaye unaegemea kwenye mali.

Amesema uwekezaji mkubwa unapaswa kuwa kwenye afya ya mwili ambayo sasa ni kwa ajili ya maisha ya baadaye, hivyo walio katika umri wa miaka 35 na kuendelea wanapaswa kuwekeza huko kwa kula mlo wenye lishe bora, kufanya mazoezi, kuepuka msongo na kulala vizuri.

Prof. Janabi ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya moyo, anayasema hayo kupitia ukurasa wake wa kijamii kuhusu maisha bora, ikiwa ni mwendelezo wa elimu kwa umma kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza (NCD) kama vile kisukari, presha na saratani.

"Wengi katika jamii hujiandaa kwa maisha ya baadaye au ya kustaafu kwa kuwekeza katika mali, hasa kujenga nyumba, ili aje akae kwake na pazuri miaka ijayo. Katika afya pia tunahitaji kuwekeza, una miaka kuanzia 35 au 40 na kuendelea unahitaji kulinda afya na kuzingatia mtindo wa maisha.

"Unywaji wa maji, ulaji matunda uwe wa kiasi gani? Ni kati ya maswali ambayo yanaulizwa sana. Unywaji maji unategemeana na shughuli ya mtu na mtu. Kunywa maji kati ya lita moja hadi moja na nusu kwa siku. Mfano, mimi binafsi mara nyingi huwa sinywi maji zaidi ya lita moja na nusu.

"Lakini wewe uko pale ofisini kuna AC umekaa tu, maji lita tatu hadi nne! Kuwe na sababu umefanya kitu, mazoezi labda hasa kipindi kama cha Desemba kuna joto kali, kwa sababu umetembea umetoka jasho umepoteza maji," anasema bingwa huyo.

Anasema unywaji maji usiozingatia uwiano wa mwili, shughuli inayofanywa na mtu huweza kusababisha maumivu ya kichwa kutokana na 'ku-dilute' sana damu na kuleta 'electrolyte imbalance' mwilini na hata kufanya moyo kwenda mbio.

"Maji ni 'solvate'. Katika miwili yetu kuna 'potassium, minerals' na kadhalika. Miili yetu pia kwa asilimia 90 ni zaidi maji, hewa na chakula. Mapigo ya moyo yako bilioni 4.5 hadi tano katika maisha yetu. Katika kila dakika lita tano za damu zinapita kwenye moyo.

"Kunywa wastani wa lita moja au 1.5 kwa siku, tembea hatua 10,000, epuka vyakula vya sukari, mafuta, kula mboga za majani na matunda katika kila mlo.

"Ulaji pia wa matunda ule wa kuchanganya matunda aina tofauti huweza kusababisha sukari kupanda. Kula aina moja kwa awamu.

"Binafsi huwa sinywi juisi iliyotengenezwa au iliyotokea viwandani, ni takribani miaka 20 tangu mwaka 2000. Sichanganyi matunda, nakula asubuhi tunda moja labda ndizi, mchana peazi na usiku kipande cha papai," anaongeza.

Prof. Janabi anasema binadamu kila anapokula anatakiwa kula kwa kiasi na kuzingatia kuepuka msongo kwa kusamehe kila anapokwazwa kama ambavyo maandiko yanaeleza kwa kuwa hali hiyo huweza kuchochea homoni ambayo husababisha hasira.

"Inakadiriwa ifikapo mwaka 2035, wengi watapoteza maisha duniani kutokana na mlo kuwasababishia NCD (magonjwa yasiyo ya kuambikiza). Watu milioni 35 kwa mwaka hufa kutokana na magonjwa ambayo hayasababishwi na bakteria, bali kutokana na wanga. Binafsi ninakula mlo mmoja kwa siku kwa miaka miwili sasa," anasema.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Mkurugenzi wa Tathmini na Ufuatiliaji wa Taasisi ya Vijana Afrika na Asia (AAYFO), Catherine Kapilima, akizungumza wakati wa uzinduzi upya wa China Media Group (CMG) na kuonyesha filamu na vipindi vya televisheni vya kichina, Dar es Salaam juzi, lengo likiwa ni kubadilishana utamaduni kati ya China na Tanzania. **PICHA: JOHN BADI**

# 'Mtaala ulioboreshwa utaleta mageuzi makubwa'

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema mtaala ulioboreshwa unaojumuisha masomo ya vitendo na ujuzi katika elimu ya sekondari, utaleta mageuzi makubwa katika sekta ya elimu nchini kwa kuwa wanafunzi watakuwa wanasoma zaidi kwa vitendo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema miongoni mwa mambo ambayo yanakwenda kufundishwa yanayotarajiwa kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na soko la ajira yanayoendana na mabadiliko ya kidunia kwa kusoma kwa vitendo ni uvuvi, kilimo, mabadiliko ya tabianchi, muziki, michezo na stadi nyinginezo.

Prof. alisema hayo juzi wakati akifunga Kongamano la Nne la Kimataifa la Ubora wa Elimu (IQEC) lililoandaliwa na Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) na kushirikisha wadau kutoka nchi za Afrika.

"Mabadiliko haya yanalenga kuwapa wanafunzi maarifa na ujuzi wa vitendo ambao ni muhimu moja kwa moja kwa tasnia hii, kuwaandaa kwa changamoto za siku za usoni na kuimarisha uwezo wao wa kuajiriwa katika soko la ajira duniani," alisema Prof. Mkenda.

Alisema kuwa ifikapo mwaka 2027, elimu ya sekondari itakuwa ya lazima kwa wanafunzi wote hadi kidato cha nne, hivyo kuashiria mabadiliko makubwa katika sera ya elimu nchini.

"Tunataka kuhakikisha kuwa wanafunzi wote ifikapo mwaka 2027/28, watakuwa na fursa ya kumaliza angalau miaka 10 ya elimu pamoja na kuongeza ujuzi wa ufundi stadi ambao ni muhimu kwa ajira halisi.

"Mtaala mpya utatoa mikondo miwili mikuu ya elimu katika shule za sekondari, mkondo wa kitaaluma wa jumla na mkondo wa ujuzi wa ufundi. Mkondo huo wa ufundi utajumuisha masomo mbalimbali kama vile uvuvi, kilimo, mabadiliko ya tabianchi na mengine mengi ambayo yatahusishwa moja kwa moja na viwanda ambavyo ni muhimu kwa uchumi wa Tanzania, muziki na michezo pia vinaunganishwa. Alisema tayari serikali imeanza kufufua shule za ufundi za zamani na inajenga nyingine mpya na kwamba shule mpya 106 za ufundi zinatarajiwa kujengwa. Lengo ni kuziba pengo kati ya kile wanafunzi wanachojifunza darasani na ujuzi ambao unahitajika katika nguvu kazi.

Mratibu wa kitaifa wa TEN/MET, Martha Makala, alisema mkutano huo umetoa mwanya kwa washiriki kujadiliana kwamba elimu bora ni hitaji la maendeleo ya kijamii na kiuchumi kama inavyoelezwa katika Ajenda ya Umoja wa Afrika 2030 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

"Tunatoa wito kwa watunga sera kushirikisha wadau kwa upana na kuzingatia michango yao katika mageuzi yote ya kisera na kisheria katika kuunda mifumo thabiti ya elimu. Hii ni pamoja na kuoanisha sera na sheria zinazohusiana na elimu na ulinzi wa mtoto kama vile Sheria ya Ndoa ya 1971 na Sheria ya Elimu ya 1978," alisema Martha.

## TCRA yatoa leseni 38 za mawasiliano miezi mitatu

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imetoa leseni 38 kwa makundi na aina tofauti za huduma katika sekta hiyo kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu.

Kati yake, leseni sita ni kwa huduma zitakazoharakisha utekelezaji mikakati ya Tanzania kujenga uchumi wa kidijitali.

Hayo yalielezwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, wakati akizungumzia hali ya mawasiliano kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu.

Alisema leseni sita mpya ni pamoja na za miundombinu ya mawasiliano, huduma za mawasiliano na programu tumizi za mawasiliano.

"Leseni moja ni ya miundombinu ya mawasiliano. Hii inamruhusu mtoa huduma kumiliki miundombinu," alisema mkurugenzi huyo na kuongeza kuwa kuna nyingine ya huduma za mawasiliano ambayo inamruhusu mwenye leseni kutoa huduma za msingi za kuunganisha mitandao mbalimbali ya mawasiliano.

"Anaweza kutumia miundombinu yake au ya mwingine.

Leseni mpya nne zimetolewa kwa programu tumizi za mawasiliano. Hizi zinawaruhusu wamiliki kuwezesha matumizi ya huduma kama vile za data ambazo zinawezesha matumizi ya intaneti.

"Takwimu zinaonesha watumiaji intaneti Tanzania wameongezeka kwa asilimia tano kati ya Julai na Septemba 2024 kutoka milioni 39.3 hadi milioni 41.1," alisema.

Aliongeza kuwa watumiaji wanakokotolewa kutokana na laini za siku zilizotumika kupata huduma ya intaneti ndani ya miezi mitatu iliyotangulia kwa kutumia teknolojia yoyote ile.

"Serikali ina lengo la kuwezesha asilimia 80 ya watu Tanzania kupata huduma za intaneti ifikapo mwishoni mwa mwaka 2025.

"Kipindi hiki TCRA pia imeidhinisha vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki 184 kutumika Tanzania. Kanuni zinataka vifaa vinavyoingia nchini kuidhinishwa. TCRA inatoa leseni za uagizaji na usambazaji vifaa vya kielektroniki," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema leseni nyingine zilizotolewa katika kipindi hicho cha robo mwaka, ni moja ya redio kimkoa, tano za redio kiwilaya, mbili za redio za jamii na tatu za huduma za televisheni za kulipiwa kitaifa.

Nyingine ni moja ya redio mtandao, moja ya kutoa huduma za kuandaa na kuchakata maudhui ya mtandaoni na blogu za habari na matukio mbili.

Takwimu limbikizi zinaonesha kuwa kufikia Septemba 2024, TCRA ilikuwa imetoa leseni 35 za miundombinu ya mawasiliano, 16 za huduma za mawasiliano na 146 za watoa huduma za programu tumizi za mawasiliano.

Leseni nyingine za huduma zilizotolewa hadi sasa ni redio 246, huduma televisheni zisizolipiwa 33 na televisheni za waya 63.

Alisema kuna televisheni za kulipia 29, televisheni mtandao 210, redio mtandao 10, blogu za habari na matukio 66 na watoa huduma za posta na usafirishaji vifurushi 146.



## DC Kaganda ataka uwazi utoaji mikopo asilimia 10

Na Jaliwason Jasson, BABATI

MKUU wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Emmanuela Kaganda, amesema mchakato wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi maalumu uwe wazi na shirikishi kwa wananchi.

Amesema mchakato huo uzingatie vikundi vyenye sifa na hatarajii kupokea malalamiko juu ya fedha hizo, bali anahitaji haki itendeke kwa kila mtu.

Kaganda alitoa agizo hilo jana wakati akitoa maelekezo ya serikali katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Babati.

"Mchakato wa utoaji wa mikopo uwe wazi na shirikishi ili mwenye sifa aweze kushiriki, sitarajii kupokea malalamiko juu ya hizi fedha," alisema Kaganda.

Aidha alisema dosari zilizokuwapo zisijirudie na kusiwapo uonevu wa kupendeleana kwa kuwa kila mwananchi mwenye sifa ana haki kupata mkopo ilimradi ana sifa.

"Watakaopata wawe kweli wanastahili kupata mikopo na madiwani tukahamasishe siyo ndugu zetu ni wale wahitaji," alisema.

Katika hatua nyingine aliwaagiza viongozi kuanzia ngazi ya chini mpaka wilaya watatue migogoro ya ardhi na siyo kuwa sehemu ya kuhamasisha migogoro ya ardhi mpaka kusababisha wataalamu washindwe kufanya kazi.

Kaganda alisema pale atakapokuta migogoro ya ardhi atasimama na sheria na kanuni katika kutatua migogoro hataangalia cheo cha mtu.

Alisema kuna sehemu zingine wataalamu wanashindwa kufanya kazi wanaenda wanashikiwa mapanga, hivyo hawawezi kuwa na utawala ndani ya utawala.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Shaaban Mpendu, alisema zaidi ya Sh. mil. 500 ndizo zimetengwa ila zilishatolewa Sh. milioni 211 na fedha wanazodai kwa watu waliokopeshwa ni Sh. milioni 80 ambapo deni hilo ni himilivu.

Diwani wa Viti Maalum, Zainab Sige aliomba madiwani kupewa miongozo ya namna ya kupata mikopo ili waweze kutoa elimu kwa wananchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Abdulaaman Kololi alisema maelekezo yote ya serikali wameyapokea na watayafanyia kazi.

# Waziri aipa kongole TANAPA ukusanyaji mzuri wa mapato

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, ameipongeza menejimenti na watumishi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), kwa kazi nzuri ya uhifadhi na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za utalii.

Alitoa pongezi hizo jana jijini Arusha, alipotembelea makao makuu ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) katika ziara yake ya kikazi.

"Mkakati wa kulinda maliasili ukiwa ndani ya eneo lako ndiyo haswa ninaoutaka na ninyi TANAPA mnatekeleza vizuri, hili unapokuwa ndani ni rahisi kuwasoma majangili natoa maelekezo kwa taasisi zote chini ya wizara kuja kujifunza TANAPA na kwenda kulitekeleza hili," alisema Balozi Chana.

Pia Dk. Chana aliziagiza taasisi zote za wizara kuzingatia maelekezo ya mawaziri nane, kuhusu utatuzi wa migogoro ya mipaka, 4R za Rais Samia na kusisitiza uadilifu kwa askari na watendaji wote na kubainisha kuwa ni jukumu kubwa la kuhifadhi ambalo walilopewa kwa niaba ya Watanzania.

Kamishna wa Uhifadhi-TANAPA, Musa Nassoro Kuji, alitoa ufafanuzi wa mafanikio mbalimbali ya shirika hilo ikiwamo juhudi zinazofanywa na TANAPA, katika kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali pamoja na wanyamapori, uboreshaji wa huduma za utalii, utekelezaji wa mfumo wa Jeshi la Uhifadhi pamoja na ukusanyaji wa mapato.

"Kwa miaka minne hadi Septemba mwaka huu, hakukuwa na tukio lolote la kuuawa kwa faru kutokana na ujangili, pia matukio ya ujangili wa tembo yamepungua kutoka 15 mwaka 2016/2017 kufikia matukio matatu katika mwaka 2023/2024," alisema.

Aidha, Kamishna Kuji, alipongeza serikali kwa kuruhusu upanuzi wa Hifadhi ya Taifa Serengeti kujumuisha eneo la Ghuba ya Speke na kulipa fidia zao wananchi walio katika kaya 3,885 sawa na asilimia 91 akisema tayari wameshaanza zoezi la kuhama kupisha shughuli za uhifadhi katika eneo hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Kasilda Mgeni (kulia), akimkabidhi kishikwambi Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Yusto Mapande (kushoto), kama kitendea kazi kwa ajili ya uwasilishaji wa taarifa za miradi ya maendeleo kwenye kata wanazoziwakilisha, mwishoni mwa wiki katika kikao cha Baraza la Madiwani. **PICHA: JAMES LANKA**

# Tuzo za uandishi habari za chakula, kilimo kufanyika

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

MTANDAO wa Vikundi vya Wakulima na Wafugaji Mkoa wa Arusha (MVIWAARUSHA) kwa kushirikiana na washirika wa mradi wa KEA (IDP, CARI) wameandaa tuzo za waandishi wa habari za masuala ya mfumo endelevu wa chakula na kilimo ikolojia.

Akizungumza jana jijini Arusha Katibu wa kamati ya tuzo hizo, Imani Hazron alisema tuzo hizo zitafanyika mwaka huu, lengo ni kutambua na kusherehekea uandishi wa habari uliotukuka kwenye masuala ya kilimo endelevu, usalama wa chakula na uendelevu wa mifumo ya chakula.

Alisema pia tuzo hizo zinalenga kuhamasisha ubora katika uandishi wa habari, kuhimiza ufuatiliaji wa kina kuhusu mbinu za kilimo cha kiikolojia na kuongeza uelewa wa umma kuhusu umuhimu wa mifumo endelevu ya chakula mbele ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la idadi ya watu.

"Waandishi wa habari watakaoshiriki tuzo hii ni wale ambao wamefundishwa na kushiriki katika kazi mbalimbali za mradi wa kilimo endelevu," alisema.


Aidha, alisema fomu za ushiriki wa tuzo hizo, zitatolewa kwenye mitandao na kwenye website yao ya https:/www.mviwaarusha.or.tz

Alisema kazi zinazostahili kupelekwa kwa ajili ya ushindani lazima ziwe zimefanyika kuanzia mwaka 2022 hadi Novemba 10 mwaka 2024.

Alisema kutokana na mafunzo yalitolewa walishirikiana na waandishi kufanya shughuli mbalimbali za usalama wa chakula na mifumo endelevu ya chakula na kilimo ikolojia.

Ezron, alisema uwasilishwaji wa kazi utakuwa wa wiki mbili kuanzia Novemba 13 hadi Novemba 28, mwaka huu.

Alisema kwenye mashindano hayo kutakuwa na tuzo lakini pia kutakuwa na zawadi nzuri ya fedha kwa kiasi kilichopangwa kama motisha ya kuendelea kufanya jitihada za kuelemisha na kuhabarisha zaidi jamii.





# Askofu KKKT aonya mafundisho potofu

**Na Remmy Moka,** MWANZA

ASKOFU mteule wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki Ziwa Victoria, Oscar Lema, amewaonya wahitimu wa mafunzo ya Biblia na kuwataka kujiepusha na mafundisho potofu.

Askofu Lema alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika mahafari ya 13 ya Chuo cha Biblia cha Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Nyakato Mwanza yaliyojumuisha wahitimu zaidi ya 30 wakiwamo wachungaji, wainjilisti na wamisheni.

Alisema wachungaji wamekuwa wakiibuka kila uchwao na kutumia vibaya mistari ya biblia wakiwapotosha waumini na kuwafanya tegemezi katika miujiza, hivyo kuwataka kutoa mafundisho yenye tija kwa taifa na waumini kwa ujumla ili kuendeleza kikazi chenye hofu ya Mungu na kinachoishi kwa kufuata misingi na taratibu.

Alisema ikiwa wahubiri wengi watapata elimu ya biblia itasaidia kuondokana na mafundisho yasiyofaa na watahubiri ukweli wa kimungu.

"Mtaonekana ni wenye tija ikiwa mtazingatia yale mliyofundishwa mkiwa hapa chuoni, huku mkijitofautisha na wahudumu wa neno la Mungu wasio kuwa na hofu ya Mungu na ambao hawajapata mafundisho ya biblia," alisema Lema.

Mkuu wa chuo hicho, Mchungaji Mimii Mziraya aliwataka wahitimu hao kutowatumia waumini kwa maslahi yao binafsi.

Alisema watumishi wa Mungu ni watu walio na wito wa kuwahudumia watu kumjua Mungu na suala la imani linawahusu watu kiroho na kimwili, hivyo jamii inaitaji watumishi wenye hofu ya Mungu.

Ofisa Taaluma wa chuo hicho, Mchungaji Lukas Shija alisema elimu hiyo waliyopatiwa wahitimu hao ililenga kuwasaidia kuendana na mazingira na kuepukana na mafundisho potofu yanayotolewa na watu wanaojiita watumishi wa Mungu.

Aidha, alisema ni vyema wahitimu hao wakatambua kuwa kwa sasa baadhi ya wahubiri wamekuwa wakihubiri injili zinazopotosha jamii ili kujiingizia kipato binafsi.

Alisema jambo hilo linasababisha watu wengi kupata mafundisho yasiyo fuata maadili ya jamii ya kitanzania, hivyo kuwataka wakatumike kwa maslahi ya taifa.

Baadhi ya wahitimu wa mafunzo hayo akiwamo, Ezekiel Kamkuru alisema mafunzo waliyopata ni moja ya fursa ya kwenda kuondoa changamoto za jamii kiroho na kimwili kwa kuzingatia maagizo ya neno la Mungu kwa kuwatoa watu gizani na kuwaleta kwenye nuru, ili wafahamu ukweli na kuepukana na mafundisho potofu.



Waandishi wa habari kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, wakipewa elimu kwa vitendo kutambua noti halali na bandia katika ofisi za tawi la Benki Kuu ya Tanzania Mwanza mwishoni mwa wiki na Ofisa Mwandamizi kutoka Kurugenzi ya Usimamizi wa Sarafu Benki Kuu, Omary Kitojo. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Sababu Watanzania kukosa fursa uwezeshwaji yatajwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi Tanzania (NEEC), Beng'i Issa, amesema asilimia kubwa ya Watanzania na wafanyabiashara hawajarasimisha shughuli zao hali inayosababisha wanakosa fursa mbalimbali za uwezeshwaji ikiwemo mikopo.

Beng'i alitoa kauli hiyo juzi mkoani Mwanza wakati akitambulisha Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wa Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA).

Hivyo kuwataka wafanyabiashara kurasimisha biashara zao ili kunufaika na fursa hizo ikiwamo mikopo na uwezeshwaji.

"Ukishafanya biashara ambayo siyo rasmi na hujasajiliwa popote huwezi kupata fursa yoyote ikiwemo mikopo wa asilimia 10 wala zabuni za serikali," alisema Beng'i.

Aidha, alisema kuna sera ya serikali inayoelekeza kuhusu asilimia 30 ya manunuzi yanayofanywa na serikali kutakiwa yafanywe kupitia makundi maalum, wanawake vijana na wenye ulemavu lakini asilimia hiyo bado haijafikiwa hata kwa asilimia tano kutokana na watu kutokuwa na shughuli rasmi.

"Ukirasimisha biashara zako unakuwa umefungua milango ya kuendelea mbele zaidi na hii ni kati ya vitu ambavyo tumeviona hivyo kuamua kuja na mafunzo ya kuwaelekeza fursa zilizopo na nini wafanye ili kuzipata ikiwemo na namna ya kutumia mitandao vyema kutokana na kila jambo linalofanyika ndani ya serikali kuhitaji kupitia kwenye mfumo," alisema Beng'i.

Aidha, alisema NEEC imeanzisha programu ya IMASA kwa lengo la kuongeza tija kwa wafanyabiahara na wajasiriamali wenye biashara zao na kuwa itawaimarisha pia wakulima katika kilimo wanachofanya.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, alisema serikali itaendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwaletea programu katika kila sekta ili waweze kuwekeza mitaji na kukua kiuchumi hususani katika shughuli za ujasiriamali.

Alisema mkoani hapa zaidi ya Sh.bilioni 5,4 zimekopeshwa kwa wavuvi kwa kuwapatia boti za kisasa na zaidi ya vikundi 35 vya ufugaji samaki kwa njia ya vizimba ambavyo vimekopeshwa kwa ajili ya kuwainua kimtaji na kuwaondoa kwenye uvuvi wa zamani na kufuga kisasa.

Alisema: "Mradi wa vijana wa unenepeshaji mifugo kwenye shamba letu la Mabuki umewawezesha vijana 35 kupata ujuzi wa ufugaji wenye tija na wameshahitimu na hivi karibuni serikali itawapatia vitalu eneo la Kitengule kwa ajili ya kufanya ufugaji".

## TAKUKURU yakaa macho kuelekea uchaguzi S/mitaa

**Na Restuta Damian,** KAGERA.

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani wa Kagera imesema inaendelea kuwafuatilia wagombea wote waliotia nia katika nafasi mbalimbali za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Imesema lengo ni kuwabaini na kuwaweka katika mikono ya sheria wote watakaojihusisha na utoaji rushwa ili kupata kura.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Kagera, Ezekia Sinkara, wakati akizungumza na vyombo vya habari mjini Bukoba juu ya taarifa mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi hiyo kwa kila kipindi cha miezi mitatu.

Sinkara alisema katika uchunguzi wao wamebani mipango na viashiria vya wanasiasa kupenyeza wagombea ambao ni machaguo yao na siyo ya wananchi na kuwa wataendelea kuchunguza kila mgombea ili kubaini matumizi ya rushwa katika uchaguzi huo.

"Ninawatahadharisha wagombea wa nafasi mbalimbali kwenye huu uchaguzi kwamba hatutasita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wale wote watakaojihusisha na rushwa lengo letu ni kuhakikisha wanapatikana viongozi chaguo la wananchi na siyo wale wanaopatikana kwa kutoa na kupokea rushwa," alisema Sinkara.

Sinkara alisema kwa kutambua kuwa wananchi wanaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka huu, ni vyema kila mwananchi akawa na elimu kupitia makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa siasa ili wasikose haki ya kuwa na kiongozi atakaesaidia kuleta maendeleo.

Katika hatua nyingine Sinkara alisema taasisi hiyo imefuatilia ujenzi wa miundombinu ya maji, wodi za hospitali, barabara, vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari na kubaini upungufu mbalimbali.

Alisema walishauri yarekebishwe na wanaendelea kufuatilia utekelezaji wa marekebisho hayo.

NIPASHE JUMATATU NOVEMBA 18, 2024
Nipashe
Spotika



MAKIPA WA4 VINARA WA KUOKOA PENALTI LIGI KUU UK. 14




JARRAD BRANTHWAITE

# MABEKI 6 WANAOWEZA KUTUA MADRID JANUARI

**MADRID, Hispania**

MWANZO wa msimu wa kusuasua kwa Real Madrid umechangiwa na jeraha baya alilopata beki wa kati, Eder Militao.

Miezi ya mwanzo ya kampeni imetawaliwa na mwanzo mgumu wa maisha ya Bernabeu kwa usajili wa majira ya kiangazi wa Kylian Mbappe na kutoswa kwa Vinicius Junior katika tuzo za Ballon d'Or, lakini kazi ya 'Los Blancos' ya kurudisha ubora wao wa kutetea mataji ya LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya imefanywa kuwa ngumu zaidi, kwa pigo aliloacha Mbrazil huyo.

Hatacheza tena msimu huu, na kumwacha Kocha Carlo Ancelotti akikosa chaguo huku David Alaba akiendelea kupata nafuu kutokana na tatizo lake la misuli.

Baada ya kumkosa Leny Yoro aliyekwenda Manchester United na kuachana na mpango wa kumsajili nahodha wa zamani Sergio Ramos, Madrid inaweza kulazimika kuingia kwenye soko la usajili Januari ili kurekebisha safu yao ya ulinzi.

Hawa hapa ni baadhi ya mabeki ambao wanaweza kuwalenga kwenye dirisha la majira ya baridi ili kukabiliana na kukosekana kwa Militao...

**#6. Jarrad Branthwaite**

Jarrad Branthwaite amelazimika kushughulika na matatizo yake ya majeraha hadi sasa msimu huu, akianza mechi mbili tu za Ligi Kuu kutokana na tatizo la paja.

Ana mambo mengi ya kufanya ikiwa anataka kuibuka kama chaguo la kweli kwa 'Los Blancos', bila shaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ni kipaji ambaye angeendana na mkakati wa Madrid wa kusajili wachezaji wachanga na wazuri.

Inaweza kuwa hatari kwa sasa ukizingatia rekodi yake ya utimamu wa mwili na akiwa bado hajaonesha kiwango cha juu, lakini bado anastahili kuzingatiwa.

**#5. Cristian Romero**

Unapojaribu kubaini safu dhabiti za ulinzi, pengine si wazo kuu kuwaangalia Tottenham Hotspur.

Hata hivyo, Spurs ina beki wa kati aliyeshinda Kombe la Dunia, Cristian Romero, ambaye inasemekana ana mashabiki wake huko Madrid.

Litakuwa jambo la kufurahisha sana kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Argentina kushirikiana na Antonio Rudiger, lakini huenda ikatakiwa kutolewa ofa kubwa zaidi Januari ili kumnasa kutoka Kaskazini mwa London.

#4. Castello Lukeba

Beki wa RB Leipzig, Castello Lukeba amekuwa mmoja wa majina ya kwanza yaliyopendekezwa na vyombo vya habari vya Hispania kupunguza jeraha la Militao.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa mara moja amejijengea sifa ya kuwa mlinzi mgumu wa upande wa kushoto, aliwasili Saxony mwaka jana akitokea Lyon baada ya Josko Gvardiol kwenda Manchester City.

Bahati mbaya kwa Madrid, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amesaini mkataba mpya wa kuongezwa na Leipzig, ambao umeongeza kifungu chake cha kuruhusiwa kuondoka hadi kufikia euro milioni 90.

Miamba hao wa Bundesliga hakika hawatataka kumuuza Lukeba kwa punguzo la fedha hiyo, na kuwaacha mabingwa hao wa Hispania katika hali ngumu ya mazungumzo.

**#3. Jonathan Tah**

Ingawa Lukeba angekuwa usajili wa gharama kutoka Ujerumani, Jonathan Tah anaweza kupatikana kwa bei nafuu zaidi.

Mkataba wa sasa wa beki huyo unamalizika mwishoni mwa msimu huu, akihusishwa na kuhamia Ligi Kuu England, huku pia akiwaniwa na Barcelona.

Bayern Munich pia wametajwa kama mahali panapotarajiwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, lakini Madrid wanaweza kuharakisha mbinu ya kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ujerumani.

**#2. Vitor Reis**

Kwa kuzingatia mafanikio ya Real Madrid katika kunyakua vijana wenye vipaji kutoka Brazil, haishangazi kwamba nyota wa Palmeiras, Vitor Reis ameibuka kama chaguo linalowezekana Januari.

Kinda huyo aliwaniwa sana na Madrid wakati wa dirisha la usajili la majira ya kiangazi na anaonekana atajiunga na magwiji hao wa Ulaya siku za usoni, baada ya kuguswa na uchezaji katika safu ya ulinzi.

Mchezaji ambaye anafananishwa na nyota wa Paris Saint-Germain, Marquinhos, Reis ni kipaji kingine cha kutumaini ambacho kinaweza kutumika kwa Ancelotti wakati wa uhitaji wake.

**#1. Laporte Aymeric**

Ramos hatarejea Bernabeu, lakini Aymeric Laporte anafikiriwa kuwa mmoja wa walengwa wakuu wa Madrid Januari.


Beki huyo wa zamani wa Manchester City hajaonesha dalili za kuruhusu viwango vyake kushuka licha ya kutimkia Saudi Arabia, akiwa na mchango mkubwa Hispania iliposhinda Euro 2024 majira ya joto.

## ISIKUPITE

INASEMEKANA kuwa Victor Osimhen, ambaye hadi sasa amefunga mabao nane na asisti nne katika mechi tisa pekee msimu huu, anafurahia muda wake huko Istanbul, akiwa na Galatasaray baada ya kujidhihirisha kama kipenzi cha mashabiki na 'hirizi' ya timu, na bado hafikirii chochote, zaidi ya mkataba wake wa sasa wa mkopo huko Chelsea ikiendelea kuhitaji saini yake.



# KANE VS WATKINS NANI ANAPASWA KUANZA ENGLAND?



KANE VS WATKINS

**LONDON, England**

KULIKUWA na hisia tofauti za kutofahamika kwa Harry Kane kuwekwa benchi Alhamisi pale jijini Athens wakati England ikicheza na Ugiriki kwenye mchezo ambao ulikuwa ni lazima washinde.

Kane ni mfungaji bora wa 'Simba Watatu' hao na alishafunga mechi za kufuzu za Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya San Marino, Bulgaria na Albania.

Lakini sasa Kane amekutana na mtu wa kucheza kamari ambaye ni kocha wa muda wa England, Lee Carsley.

Bosi huyo wa muda wa England alimwacha nahodha wake benchi Alhamisi usiku kwa mchezo ambao ulikuwa na umuhimu zaidi kushinda dhidi ya Ugiriki, na badala yake akamchagua Ollie Watkins wa Aston Villa kuanza kama mshambuliaji kiongozi.

Ni uamuzi ambao Carsley alisema kuwa Kane alikuwa nao "sawa kabisa", ingawa mshambuliaji huyo wa Bayern Munich anaweza kuwa alikuwa akiugulia moyoni wakati alipokuwa akitazama mchezo huo huku Watkins akifunga bao la kwanza kwa njia ya kuvutia katika ushindi mnono wa mabao 3-0.

Ilionekana kwamba England ingeweza kuishinda Ugiriki bila mshambuliaji wao huyo mahiri.

Lakini uchezaji wa Watkins kule Athens ulizua swali ikiwa anafaa kuwa kiongozi wa safu ya ushambuliaji ya Simba Watatu hao wakati Thomas Tuchel atakapochukua jukumu la kuwa kocha mkuu wa kikosi cha England 2025.

Sasa, makala haya yanakuchambulia ulinganisho wa washambuliaji hao wawili, na tathmini ya nani anafaa kuanza kwa kikosi cha England.

### Kufunga mabao

Bao la Watkins, Alhamisi lilikuwa la tano kwake kuifungia timu ya taifa katika michezo 18, na lilikuwa aina ya bao ambalo tumezoea kuliona likifungwa na Kane kwa miaka mingi.

Fowadi huyo wa Villa alijiweka sawa na kupiga mkwaju kwa urahisi akitumia vizuri asisti ya mlinzi Noni Madueke.

Watkins ana wastani wa kufunga bao kila baada ya dakika 121.2 kwa Simba Watatu hao, huku mfungaji bora wa muda wote wa England, kwa wastani, akifunga kila baada ya dakika 115.9. Hii ni rekodi ya Kane aliyofunga mabao 68 katika mechi 102 ambayo ni bora.

Kuna wachache bora kuliko Kane. Alikuwa anainyemelea rekodi ya Alan Shearer ya kufunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu England kabla ya kuondoka kwenda Bayern Munich, ambapo alifunga mabao 36 ya Bundesliga katika kampeni yake ya kwanza.

Watkins alifunga mabao mengi zaidi katika msimu mmoja wa mabao 19 (2023/24) na aliongoza kwa mara ya kwanza mbele ya Kane ambaye alimwongoza mara saba.

Fowadi wa Bayern ni mpiga mpira wa kutisha ambaye huwa sahihi kutoka miguu yote miwili. Yeye ni gwiji katika eneo la penalti na mmoja wa wachezaji bora kwenye yadi 12.

Katika msimu mmoja tu kati ya misimu nane iliyopita ya ligi, Kane alifunga chini ya kiwango chake cha mabao msimu wa (2021/22), kwa mujibu wa FBref.com

Tofauti na Watkins, ambaye amefanya vibaya katika misimu minne kati ya saba.

Uchezaji wake wa juu zaidi ni msimu uliopita, wakati Kane amekuwa bora kwa misimu saba mfululizo.

Ingawa Watkins amefanya vema katika umaliziaji na ni mzuri sana anapopiga mpira kutoka pembeni, yeye si mfungaji bora kama Kane.

### Umiliki wa mchezo na ubunifu

Msimu wa Watkins wa mabao 19 wa Ligi Kuu England wa 2023/24 ulifanywa kuwa wa kuvutia zaidi kwake.

Nyota huyo muhimu wa Kocha Mkuu wa Villa, Unai Emery, aliongeza pasi 13 za mabao kwenye hesabu yake ya kuhusika kwenye mabao msimu huo.

Na ndio rekodi bora zaidi kwa msimu mmoja katika maisha yake ya soka hadi sasa.

Mara moja tu Kane ameboresha takwimu hiyo. Alirekodi asisti 14 kwenye ligi msimu wa 2020/21 wakati huo akicheza kwa upatina mzuri na Son Heung-min aliyekuwa kwenye kilele chake cha ubora.

Kane anacheza vema akiwa nyuma ya goli na bila shaka anajivunia upigaji pasi wa hali ya juu.

Amekuwa akicheza kama namba 10 katika miaka michache iliyopita, huku mielekeo yake mikali ikielekea kwenye lango la wapinzani na alionekana kuifurahia nafasi hiyo.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur pia ni gwiji wa kushinda faulo. Kwa hiyo mara nyingi anaweza kuipa timu yake ahueni kwa kupata mipira ya adhabu.

Watkins anaimarika kama mwezeshaji, kwa uwezo wake wa kujipanua pembeni na kufungua nafasi kwa wachezaji wenzake na sehemu kubwa ya uchezaji wake si wa moja kwa moja.

Mshambuliaji huyo alisaidia kwa njia nyingi msimu uliopita, huku aina mbalimbali za onesho zikielezea mabadiliko ya Watkins.

Nyota huyo wa Villa ni mchezaji anayeanza kuibuka kama mbunifu, lakini uthabiti wa Kane katika nyanja hizi kwa miaka mingi inamaanisha lazima atahitaji muda zaidi kujifunza.

### Maisha marefu

Enzi ya Tuchel inaelekezwa kuelekea Kombe la Dunia la 2026, na hilo ndilo tunalotazamia katika mjadala wa Kane dhidi ya Watkins.

Hadi michuano hiyo itakapoanza Juni 11, 2025, Kane atakuwa na umri wa miaka 32 na atafikisha miaka 33 baada tu ya michuano hiyo.

Umri si jambo la kusumbua sana, huku mshambuliaji huyo akiwa na matumaini ya kufurahia kazi ndefu.

Hata hivyo, kutokana na idadi kubwa ya michezo ambayo amecheza tangu akiwa Tottenham katika miaka yake ya mapema ya 20 na kuzorota kimwili kulikodhihirika kwenye michuano mikubwa, kuna wasiwasi kuhusu hali ya afya ya Kane kufikia Kombe la Dunia la 2026.

Kwa ujumla Kane amekuwa akisumbuliwa na jeraha katika miaka ya hivi karibuni kutokana na matatizo ya kifundo cha mguu wakati wa Kocha Mauricio Pochettino akiwa Spurs, lakini hakuna ubishi kwamba idadi ya dakika anazocheza msimu mzima huleta mchango mkubwa.

Kwa mara ya kwanza kabisa, Gareth Southgate alikuwa tayari kumuacha Kane ili kumpa nafasi Watkins kwenye Euro 2024.

Mshambuliaji huyo alikuwa akikabiliana na tatizo la maumivu ya mgongo kipindi cha majira ya joto.

Watkins ni mdogo kwa Kane kwa miaka mitatu, lakini atakuwa na miaka 30 mwanzoni mwa Kombe la Dunia la 2026.

Siku hizi, huo si umri wa kuwa na wasiwasi kuhusu kudhoofika kimwili, lakini ataweza kuwa katika ufanisi kwenye kufanya kile ambacho kinatakiwa?

Huenda ikabidi kuwe na mageuzi katika mchezo wa mshambuliaji huyo ikiwa anataka kufanya vema katika kiwango cha juu kwenye miaka yake ya 30.

Kwa washambuliaji wote wawili, usimamizi kwao utakuwa muhimu ili kuingia kwenye mashindano.

Hakuna sababu ya kuamini kuwa Kane atadhoofika sana kimwili katika kipindi chote cha mzunguko wa Kombe la Dunia, lakini huu unaweza ukawa ndio mwisho wake kama mchezaji mkuu wa England.

### Nani anafaa zaidi kwa Tuchel?

Hili ndilo swali muhimu na gumu. Kane ni mshambuliaji bora kuliko Watkins, lakini je, yuko vizuri kimbinu kwa timu hii ya England?

Kwa mfano kwenye Euro 2024, Southgate alihangaika sana kupata usawa na ubora wa Kane akimchezesha na Jude Bellingham, lakini ilionekana kama alikosekana mtu wa kulisha mipira mbele ya nusu mstari.

Watkins anaweza kufanya vipengele vya kile Kane anafanya kwa mtazamo wa kumiliki mpira na ubunifu, na nia yake ya kunyosha uwanja kwa kufungua nafasi kwa wachezaji wa England kung'ara.

Kwa kuzingatia mfumo wa Tuchel, Watkins ataweza kuwalisha vizuri zaidi mipira wachezaji kama Bellingham, Cole Palmer na Bukayo Saka, hivyo nyota huyo wa Vila bila shaka ni chaguo la kuvutia.

Hata hivyo, kocha anayekuja wa England pia anajua hatari ya Kane atakapopewa mkimbiaji wa kumlisha mpira mbele.

Kama Anthony Gordon angepata nafasi zaidi kwenye michuano ya Euro, uchezaji wa Kane hakika ungeboreshwa huku kikosi cha Southgate kingekuwa na nguvu zaidi upande wa kushoto.

Tuchel tayari amefanya kazi na Kane huko Bayern. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alitikisa nyavu mara 44 katika mashindano yote msimu uliopita.

Kane anatazamia kufanya kazi tena na Mjerumani huyo, huku Tuchel akiendelea kumpigia debe fowadi huyo wakati alipokuwa Bavaria, akieleza kuwa ni 'hatari' kumfundisha Kane.

Kuzoeana huku kunamaanisha kuwa Tuchel atajaribu kumfanya Kane kuwa wa kwanza kwake kabla ya kumgeukia Watkins.

## Nukuu

"Namtakia Ruben Amorim kila la kheri duniani kwa sababu Manchester inalihitaji hilo," **Cristiano Ronaldo baada ya kufunga mara mbili Ijumaa wakati Ureno ikishinda mabao 5-1 dhidi ya Poland. Amorim ambaye naye ni raia wa Ureno ametua kuinoa United wiki iliyopita akitokea Sporting CP ya nchini humo.**



"Siku zote kutakuwa na uvumi na sasa Januari inakaribia, itakuwa pia, lakini sipotezi nguvu kwa kelele za nje, nimefurahishwa na jinsi ninavyoishughulikia na nitaishughulikia." **Kiungo wa Real Sociedad, Martin Zubimendi, ambaye anawindwa na Arsenal na Manchester City.**



"Tunajua itachukua muda na tutajaribu kushinda wakati na michezo. Lakini tunapaswa kuanza tangu siku ya kwanza bila hofu, bila kufikiria kuwa hawajazoea kucheza hivi. Hili haliniingii akilini. Wataanza siku ya kwanza na wazo letu, haijalishi ndio lengo," **Kocha mpya wa Manchester United, Ruben Amorim, katika mahojiano yake siku ya kwanza akianza kazi katika klabu hiyo.**



Nipashe Spotika

NIPASHE JUMATATU NOVEMBA 18, 2024



Kipa wa Tabora United, Hussein Masalanga, ambaye alidaka penalti ya Stephane Aziz Ki, Novemba 7, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam. . **PICHA: MTANDAO**

# MAKIPA WA4 VINARA WA KUOKOA PENALTI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya penalti 25 zimepatikana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea msimu huu wa 2024/25, hadi kufikia raundi ya 10 na baadhi ya mechi za raundi ya 11.

Kati ya penalti hizo, 19 zimewekwa ndani ya nyavu na sita zikikoswa. Penalti zilizokoswa, mbili ziliota mbawa kwa kutoka nje huku nne zikiokolewa na magolikipa.

Mbili zilizoota mbawa zilipigwa na Amza Mubarack wa Namungo, Agosti 29, mwaka huu, Uwanja wa Majaliwa uliopo Ruangwa, Lindi, timu yake ikipoteza nyumbani kwa mabao 2-0 dhidi ya Fountain Gate, na Heritier Makambo wa Tabora United ilipocheza dhidi ya Fountain Gate na kubugizwa mabao 3-1, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora, Septemba 20, mwaka huu.

Wafuatao ni makipa waliookoa penalti nne kwenye Ligi Kuu na wachezaji ambao walipizipiga...

**1# Ley Matampi - Coastal Union**

Ley Matampi wa Coastal Union, raia wa Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo, aliokoa penalti ya Djuma Shaaban, katika mchezo ambao timu yake ilicheza dhidi ya Namungo, Septemba 17, mwaka huu, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam.

Antony Mlingo alifanyiwa madhambi ndani ya eneo la hatari. Djuma alipiga kwa mguu wa kulia upande wa kushoto mwa kipa huyo. Aliruka upande huo huo na kuupangua, ukaenda kugonga mwamba wa juu.

Kwa bahati mbaya sana mabeki wa Coastal wakashinda kuuwahi na Paul Buswita akaumalizia wavuni kwa mguu wa kushoto na kuwa bao la pili kwenye mechi hiyo iliyoisha kwa Namungo kushinda mabao 2-0.

Matampi tayari alikuwa ameshafanya kazi yake ya kuokoa penalti, bao lililofungwa halikuwa la tuta badala yake lilihesabika kuwa la kawaida.

**2# Metacha Mnata - Singida Black Stars**

Golikipa wa Singida Black Stars, Metacha Mnata alicheza penalti ya Hassan Dilunga wa JKT Tanzania, wakati timu zao zilipokutana, Septemba 29, mwaka huu, Uwanja wa Liti Singida na kutoka sare ya bao 1-1.

Ismail Aziz, aliangushwa ndani ya kisanduku cha hatari na mwamuzi kutoa tuta. Alipiga kwa mguu wa kulia, mpira ukaenda upande wa kushoto ambako Metacha alikuwa ameruka, akaupangua, na kuudhibiti.

**3# Ramadhani Chalamanda - Kagera Sugar**

Kipa Ramadhani Chalamanda, aliokoa penalti ya Maabad Maulid wa Coastal Union, Septemba 29, mwaka huu, katika mchezo uliopigwa, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, ambao timu yake ya Kagera Sugar ilipoteza kwa bao 1-0.

Alikuwa ni Omari Chibada, aliyeunawa mpira ndani ya boksi. Maabad kwa kutumia mguu wa kulia alipiga mpira upande wa kushoto kwa kipa huyo wa Kagera Sugar, akaruka, akaupangua, mmoja wa wachezaji wa Coastal Union aliuwahi kutaka kufunga, lakini akapaisha juu.

**4. Hussein Masalanga - Tabora United**

Ilikuwa ni Novemba 7, mwaka huu, wakati Hussein Masalanga, alipoidaka penalti ya Stephane Aziz Ki, wakati timu yake ya Tabora United, ilipoibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Yanga, mchezo ukipigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Wakati makipa wenzake wakipangua, kipa huyu ameweka rekodi yake ya kuudaka kabisa penalti hiyo na ndiye kwa kiasi kikubwa aliyesababisha kupatikana bao la pili kwa timu yake.

Pacome Zouzoua, aliangushwa ndani ya kisanduku cha hatari, ikaamriwa lipigwe tuta wakati huo Yanga ikiwa nyuma kwa bao 1-0.

Aziz Ki, alipigwa kwa mguu wa kushoto na kuupeleka kushoto kwa kipa huyo, ambaye aliruka na kuukamata. Alinyanyuka nao na kuupiga mbele kwa Yacouba Songne kwenye wingi ya kushoto, akamwacha Denis Nkane na kutoa krosi kwa Offen Chikola aliyeukwamisha wavuni.

Ikumbukwe kuwa matukio hayo yalitokea ndani ya dakika moja kutoka upigaji penalti, kipa kuudaka na kwenda kuzaa bao la pili.

**JE, WAJUA?**



MFUNGAJI bora wa muda wote wa England, Harry Kane, anashikilia rekodi hiyo kwa mabao yake 68 katika mechi 102, kwa wastani akifunga kila baada ya dakika 115.9. Hii ni kabla ya mechi ya jana ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya dhidi ya Iceland.





## Mavunde apewa tuzo kutambua mchango wanawake

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

JUKWAA la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Mkoa wa Dodoma limemkabidhi tuzo Waziri wa Madini na Mbunge wa Dodoma Mjini, Antony Mavunde ya kutambua mchango anaotoa kwa wanawake ili kujiinua kiuchumi.

Tuzo hiyo ilitolewa jijini juzi na mlezi wa jukwaa hilo, Tunu Pinda wakati wa kongamano la kuipongeza serikali pamoja na utoaji elimu ya kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali ili kupanua wigo wa ubunifu kwenye ujasiriamali.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo, Mavunde aliwataka wanawake kutumia fursa zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan hususani mikopo ya asilimia 10 kubuni biashara mbalimbali ili waweze kuondokana na umaskini.

Alisema hivi sasa wanawake wanatakiwa kuondoka kwenye utengenezaji badala yake kubuni biashara zenye mtazamo wa kimataifa ili wapige hatua zaidi na kuingia kwenye soko la ushindani.

"Fursa zilizopo mkoani Dodoma ni nyingi mno hivyo ni nyie kupanga mnafanya kitu gani ambacho kitawainua kiuchumi nisingependa kusikia kila siku mnafanya biashara ya batiki peke yake," alisema Mavunde.

Aidha alisema serikali imerudisha mikopo ya kinamama ya asilimia 10 ikiwemo Sheria ya Manunuzi ya Umma imefanyiwa marekebisho ili taasisi nunuzi zitenge asilimia 30 ya manunuzi yake kwa ajili ya makundi maalum likiwamo la kinamama.

Alisema ataendelea kuwawezesha kiuchumi wanawake kwa vitendo na kwa kuanzia anatarajia kuwakabidhi mitambo ya kusafishia mafuta ya alizeti kinamama wa kikundi cha Ipagala ikiwa ni sehemu ya ahadi ya uanzishwaji wa kiwanda cha kuongeza thamani mazao.

"Nitaendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi lengo ni kuona wanapiga hatua katika ujasiriamali wanaofanya," alisema Mavunde.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuona kundi la wanawake likinufaika kupitia sheria na sera wezeshi.

# Wenye ulemavu wanolewa matumizi mfumo wa NeST

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imetoa mafunzo kwa watu wenye ulemavu ya kuwajengea uwezo wa matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa manunuzi ya umma (NeST), ili kuwawezesha kunufaika na fursa zilizoko kwenye zabuni za umma.

Mkurugenzi wa Idara ya Wenye Ulemavu Ofisi ya Waziri Mkuu, Rashid Maftah, akifungua mafunzo hayo juzi jijini hapa aliwataka washiriki kushiriki kikamilifu ili kupata uelewa wa kutosha juu ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na Matumizi ya Mfumo NeST.

Alisema mafunzo hayo yatalisaidia kundi hilo la walemavu nchini kupata uelewa wa kutosha kuhusu fursa zilizopo kwenye sheria hiyo ambayo inasimamia zabuni za umma.

"Niwaombe watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu ili mpate uelewa wa kutosha juu ya Sheria ya Manunuzi ya Umma pamoja na mfumo huu wa NeST ambao mtautumia kupata zabuni za serikali kwa mujibu wa sheria," alisema.

Aidha, alisema kutoka na ujio wa sheria mpya ya ununuzi wa umma hakutakuwa na utaratibu wa kuomba zabuni za serikali nje ya mfumo, hivyo mafunzo hayo yamekuja wakati mwafaka kuliwezesha kundi hilo kunufaika na fursa hiyo.

"Mafunzo haya yatawawezesha watu wenye ulemavu kupata fursa ya kuomba zabuni za serikali na kujipatia ajira na kuajiri wengine na kuondokana na umaskini," alisema Maftah.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Salmin Malole, alisema katika kipindi cha miaka mitatu serikali imefanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya ununuzi wa umma.

"Kwanza kwa kujenga mfumo wa NeST na pia kuwezesha kuwapo kwa sheria mpya ya ununuzi wa umma yaani Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 na kanuni zake za mwaka 2024, yote haya yameongeza wigo wa fursa kwa Watanzania na kurahisisha upatikanaji wake kwa uwazi na usawa," alisema.

Alisema mafunzo hayo yanafanyika ikiwa ni mwendelezo wa programu ya PPRA ya kuwajengea uwezo wadau wa ununuzi wa umma yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

"Serikali kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, imetoa fursa ya upendeleo maalum kwa Watanzania wote. Lakini pamoja na upendeleo wa aina mbalimbali ulitolewa kuna upendeleo wa makundi maalum ambayo ni vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu," alisema.

Alisema sheria hiyo ambayo PPRA wanaisimamia utekelezaji wake inazitaka taasisi za serikali kutenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi kwa ajili ya makundi maalum.

"Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya serikali iliyoko madarakani ambayo iliahidi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 kuwa itaongeza ajira na kuwainua wananchi kiuchumi," alisema.

Alisema ajira hizo zinapatikana sasa kupitia fursa za zabuni za umma kwa Watanzania hata wasio na kampuni.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kuhusu rufani za wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi ngazi ya serikali za mitaa waliokatiwa kuwa wamerudishiwa haki yao ya kugombea. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Polisi yawaonya wafanya vurugu uchaguzi S/mitaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, amesema hawatamfumbia macho mtu yeyote ambaye anataonekana kuwa na nia ya kufanya vurugu ili kuharibu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Katabazi alisema hayo juzi jijini hapa akizungumza na wakazi wa jijini Dodoma baada ya kuhitimisha matembezi ya kilomita sita yenye lengo la kuhamasisha watu kufanya mazoezi ili kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema kuelekea uchaguzi huo jeshi hilo litahakikisha linaimarisha ulinzi na usalama ili kila mtu ashiriki mchakato wa uchaguzi kwa amani.

Alisema wananchi wanatakiwa kutambua kuwa suala la kulinda amani ni jukumu la kila mtu na siyo Jeshi la Polisi pekee.

"Tunatakiwa kutambua kuwa ulinzi na usalama unaanzia kwa mtu mmoja, familia pamoja na jamii kwa ujumla wake na Jeshi la Polisi lipo kwa ajili ya kuimarisha ulinzi zaidi.

"Tunatambua kuwa polisi siyo adui kwa raia na kuna umuhimu mkubwa katika kushirikiana lakini itakapotokea mtu akaonekana kuvuruga amani hapo mtu huyo kamwe hatutamvumilia," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliagiza kuundwa kwa vikundi vya kufanya mazoezi katika mitaa yote ili kusaidia kukabiliana na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza nchini.

Alisema: "Mazoezi ni sehemu muhimu ya kujenga afya na kumfanya mtu kuepukana na kupata magonjwa yasiyo ya kuambukiza, hivyo Watanzania tunapaswa kujenga mazoea ya kufanya mazoezi mara kwa mara".





# Watu 23 mbaroni tuhuma mauaji, ubakaji, kuvunja

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe limewakamata watuhumiwa 23 wa makosa mbalimbali ikiwamo, uvunjaji, wizi, mauaji pamoja na ubakaji.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Banga alisema kukamatwa kwa watu hao ni kufuatia kufanyika kwa operesheni iliyofanywa na jeshi hilo kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Novemba mwaka huu.

Alisema kwa upande wa usalama barabarani pia jeshi hilo limezuia makosa mbalimbali ya ajali kwa kutoa elimu kwa madereva na wamiliki wa vyombo vya moto pamoja na wananchi.

"Jumla ya madereva 5, 921 walikamatwa, waliofikishwa mahakamani mmoja lakini waliopewa onyo 10 na walioandikiwa faini ni 5, 920 na waliofungiwa leseni walikuwa wawili," alisema Banga.

Wakati huo huo, Kamanda Banga alitoa wito kwa wananchi mkoani Njombe kuwa watulivu katika kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Jeshi la Polisi litaendelea kutoa ulinzi kwa vyama vyote, wakati wa kampeni na kuhakikisha kwamba wakati wote wa kampeni na siku ya kupiga kura basi kuwa na amani na utulivu kwa sababu tumejipanga vilivyo," alisema Banga.

Kadhalika, Kamanda Banga alitoa rai kwa wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutoa taarifa za uhalifu ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wale wote ambao wanatenda makosa ya kihalifu.

Nao baadhi ya wananchi Mjini Njombe, Laulian Sanga alisema Jeshi la Polisi linapaswa kuendelea kutoa elimu kwa madereva sambamba na kuchukua hatua kali kwa wale ambao hawafuati sheria pindi wawapo barabarani.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Mbunge wa Ileje, Godfrey Kasekenya, akisisitiza jambo kwa wazee wa Ileje, mkoani Songwe alipokagua miradi ya maendeleo jimboni kwake juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Njombe yapanga kukusanya mapato bil.4.7/-

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, limepanga kukusanya Sh. bilioni 4.7 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Vasco Mgunda, wakati akifungua baraza la madiwani lililofanyika katika ukumbi wa halmashauri hiyo Kidegembye.

Mgunda alisema hadi kufikia Septemba mwaka huu halmashauri imefanikiwa kukusanya shilingi milioni 912.2 sawa na asilimia 19.

"Kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, halmashauri imetengewa jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 9.3 ambapo kiasi cha shilingi bilioni tatu imetengwa kutoka serikali kuu na shilingi milioni 4.3 ni fedha kutoka kwa wafadhili na kiasi cha shilingi milioni 1.9 ni fedha kutoka mapato ya ndani," alisema Mgunda.

Alisema halmashauri kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 imevuka lengo kwa kukusanya kiasi cha bilioni 3.7 ambazo zimetumika kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

"Katika kipindi cha mwezi Julai Mosi hadi Septemba 30, mwaka huu, jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 2.1 sawa na asilimia 20.6 ya makisio ya fedha za miradi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye maendeo mbalimbali ya halmashauri yetu," alisema Mgunda.

Hata hivyo alisema halmashauri inaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ili kuboresha huduma za afya kuanzia ngazi ya halmashauri, kata na vijiji ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora pamoja na kuwapunguzia umbali.

Kwa upande wake mkaguzi wa ndani kutoka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Reagan Mroso alisema pamoja na kufanya vizuri upande wa mapato lakini bado kuna tatizo kwa robo mwaka bado hawajaweza kufikia asilimia 25.

"Tupo asilimia 19 kwa hiyo tunaelekezwa kuelekeza juhudi katika vyanzo vyote vya mapato, tusimamie vizuri katika ukusanyaji nna sasa watendaji kama mpo hapa tuhakikishe hatupotezi mapato," alisema Mroso.

Nao baadhi ya madiwani, akiwamo Innocent Gwivaha alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Christopher Sanga kwenda nchini China kujifunza ili kuanzisha miradi ya viwanda visivyopungua viwili vya kuchakata parachichi ili kuzalisha mafuta ya kupikia pamoja na vyakula vya mifugo.

Alisema lengo ni kukabiliana na mlipuko wa bei ya mafuta ya kupikia ambao hujitokeza mara kwa mara.

Gwivaha alisema uazishwaji wa viwanda utasaidia pia halmashauri kuongeza mapato sambamba na kukuza uchumi wa wananchi kupitia vijana kupata ajira.

# Wanaoishi mazingira magumu wapewa umeme jua

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WANANCHI zaidi ya 250 wanaoishi katika mazingira magumu wakiwamo wenye ulemavu pamoja na watoto yatima wilayani Makete Mkoa wa Njombe, wamepewa msaada wa nishati ya umeme wa jua kutoka nchini Sweden wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 20.

Msaada huo ulitolewa mwishoni mwa wiki katika kituo cha kulea watoto yatima Bulongwa ambacho kipo chini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini Kati.

Akizungumza kwa niaba ya Askofu wa Kanisa la Kiinjili Kilutheri Tanzania Dayosisi ya Kusini Kati, Wilson Sanga, Mkuu wa Jimbo la Kati Bulongwa, Mchungaji Adrick Mwambemba alisema kuwa msaada huo utawasaidia walengwa kumtumikia Mungu pamoja kukuza uchumi wao.

"Kazi ya nuru ni kuwaongoza watu kutenda mema na siyo kutenda mabaya, nyinyi wenzetu mliopewa vifaa hivyo kazi yenu ni kuangaza na kazi ya pili ya nuru ni kutoa hofu," alisema Mwambemba.

Mlezi Mkuu wa makao ya watoto yatima Bulongwa, Vaileth Chaula alisema kuwa wamisionari kutoka nchini Sweden pamoja na msaada huo wamekuwa wakitoa pia misaada katika kituo hicho cha watoto yatima tangu mwaka 1990.

Alisema: "Wafadhili wa makao ya watoto Bulongwa kutoka nchini Sweden wametusaidia mwanga vijijini kwa wenye uhitaji wakiwamo, watoto yatima, walemavu na wazee ambao hawana mwanga nyumbani mwao," alisema Vaileth.

Mwakilishi wa Chama cha Semu kutoka nchini Sweden, Hannes Sandahl alisema wataendelea kushirikiana na wakazi wa Makete kupunguza matatizo katika jamii.

Baadhi ya wanufaika wa mradi huo akiwemo, Anna Nyondo alisema msaada huo utawasaidia kuondokana na giza pamoja na kukuza uchumi wao.

Hata hivyo nishati hiyo ya jua zenye mfumo wa taa na redio zimefungwa kwenye kaya 50 wilayani Makete ambapo inakadiriwa kuwa watu zaidi ya 250 wanatarajia kunufaika na msaada huo ambao umetolewa na Chama cha Kimisionari cha Semu kutoka nchini Sweden.



## Waziri aingilia mgogoro wa njia, atoa maagizo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi Zanzibar, Shaban Ali Othman, amelitaka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Zanzibar katika shehia ya Buyu kusafisha njia ambayo wanatumia wakulima wa mwani kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kila siku.

Aliyasema hayo jana wakati alipofanya ziara ya kuangalia eneo lenye mgogoro wa njia baada ya kupata malalamiko kwa wananchi wanaoendesha shughuli za uvuvi na ukulima wa mwani.

Waziri Shabani alisema kuwapo kwa njia ya ukakika ni jambo jema kwa wananchi kupita kutokana na kuwasaidia wakulima wa mwani pamoja na watumiaji wengine wa eneo hilo jambo ambalo litaondoa migogoro.

Naye Naibu Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto, Mrisho Iddi Mbaraka, alisema wamepokea ushauri huo na wapo tayari kuufanyia kazi kwa ajili ya usalama.

Diwani wa Wadi ya Chukwani, Fatma Rashid Juma, aliwataka wakulima wa mwani wa eneo hilo kutoa ushirikiano wa pamoja katika utatuzi wa matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika eneo hilo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uvuvi, Chukwani Ramadhan Khamis, aliwataka wakulima hao kuwa walinzi baada ya kukamilika kwa njia hiyo ili kudhibiti vitendo vya uhalifu visijitokeze katika eneo hilo.

Wakulima wa mwani wa eneo hilo walisema hatua ya waziri huyo kufika katika eneo hilo na kusuluhisha mgogoro huo kutaleta hari na hamasa ya kufanya kazi zao za ukulima wa mwani bila ya usumbufu.

# Bodaboda chanzo ongezeko ajali barabarani Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohammed, amesema ongezeko la ajali za barabarani linatokana na mwendokasi hasa kwa madereva wa bodaboda ambao wengi wao hawafuati sheria na wanaendesha kwa mihemko.

Alisema licha ya serikali kuchukua jitihada za kudhibiti bado kuna ongezeko la ajali hizo kwa sababu baadhi ya madereva ni wagumu kufuata sheria na kanuni zilizoko.

Aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Usalama Barabarani iliyofanyika Mjini Unguja.

Alisema watu wengi wanadhana kuwa suala la usalama barabarani ni la wizara husika na Jeshi la Polisi jambo ambalo siyo sahihi.

Alisema maadhimisho hayo hayatoshi kuwa suluhisho la ajali za barabarani, jambo la msingi ni kukaa na kutafakari juu ya nini kifanyike.

Alisema kuna malalamiko mengi wakilalamikiwa madereva wanaoendesha gari za watembeza watalii ambao huendesha kwa mwendo wa kasi.

"Kila mtu anafahamu kuendesha gari kwa mwendo wa kasi au kutumia kilevi ni kosa na kinyume na utaratibu lakini haya yamekua yakitokea, wizara itakua wakali juu ya jambo hili," alisema.

Dk. Khalid alisema hivi sasa serikali imekuja na suala la mtandao wa barabara na kuzisajili barabara zote kuwa bora kwa upande wa Unguja na Pemba.

Waziri huyo alisema kujengwa kwa barabara za kisasa ni kuiweka Zanzibar kuwa na haiba nzuri lakini jambo la kushangaa baada ya kujengwa barabara hizo wananchi huweka matuta barabarani na huziharibu.

Alisema kwa kawaida barabara huwekwa matuta na wizara husika kama kuna haja ya kufanya hivyo ikiwamo maeneo ya ibada, shule, masoko na sehemu zenye mikusanyiko ya watu na siyo sehemu yoyote.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Habiba Hassan, alisema kwa mara ya kwanza wiki ya usalama barabarani inafanyika Zanzibar kutokana na matakwa ya mkataba ya sheria kwa nchi za Afrika kuja na wazo la kuanzishwa wiki hiyo.

Akitoa taarifa ya ajali za barabarani Zanzibar kwa mwaka 2023-2024 Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mjini Magharibi, Khamis Mwakanolo alisema kwa mwaka 2023 kuanzia Januari hadi Septemba ni ajali 142 zimeripotiwa.

Alisema kwa mwaka 2024 ajali 174 zilitokea huku vifo vitokanavyo na ajali hizo kwa mwaka 2023 ni 101 na kwa mwaka 2024 ni 134 na kufanya kuwa ongezeke kubwa la vifo vinavyotokana na ajali za barabarani.

Alisema ajali nyingi zilizoripotiwa zinatokana na makosa ya kibinadamu yanayotokana na mwendo kasi sambamba na madereva wengi kutokuwa na leseni.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani Kamisheni ya Zanzibar kimeweka mikakati kadhaa ikiwamo kubaini maeneo tete ambayo yanatokezea ajali mara kwa mara ili kuchukua hatua.

Mwenyekiti wa Kitaifa wa Jumuiya ya Usafiri Barabarani Zanzibar, Haroub Soud Mzee alisema licha ya serikali kuweka mikakati imara ya kudhibiti ajali za barabarani ipo haja kuwekwa adhabu mbadala hasa kwa waendesha bodaboda ikiwamo kuchapwa viboko hadharani.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (katikati), akipokea vitendea kazi vya ofisi ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda (kushoto), baada ya kuhitimisha ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria katika usimamizi wa Utumishi wa Umma jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# COSOZA kuwathamini, kuwajali wasanii wakongwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Msajili wa Haki Miliki Zanzibar (COSOZA) imesema itaendelea kuwathamini na kuwajali wasanii wakongwe na wabunifu kwa sababu wametoa mchango mkubwa kuitangaza Zanzibar nje ya Tanzania.

Akizungumza baada ya kuwatembelea wasanii na wabunifu wakongwe visiwani humo, Ofisa Mkuu Divisheni kutoka ofisi hiyo, Haji Sungura Makame, alisema kuwa lengo na kufanya kazi hiyo ni kuwajali wakongwe hao kutokana na mchango wao mkubwa kwa maendeleo ya Zanzibar.

Alisema wasanii hao wakongwe wameacha kazi zao na kuifanya sanaa ya Zanzibar kama njia moja ya kuitangaza nchi kupitia kazi zao za sanaa.

"Tumekuwa na utaratibu huu wa kila mwaka kuwatembelea wazee wetu hao kwa sasa ni wagonjwa na wamefanya kazi kubwa ya sanaa kuitangaza Zanzibar," alisema.

Alisema kuwa ofisi hiyo imejipanga katika kuhakikisha kuwa wasanii wakongwe wa sanaa za maigizo na wabunifu wanaendelea kutazamwa wakati wakiwa wagonjwa na kupatiwa misaada mbalimbali.

Alisema kuwa licha ya taasisi hiyo kufanya ziara na kuwatembelea kwa wakongwe hao bado jitihada zinahitajika kwa taasisi nyingine kuwaangalia watu hao na kuwafariji kwa sababu walikuwa kioo cha jamii.

Naye msanii wa maigizo, Jazaa Hamadi (bitele) alisema kuwa licha ya kufanya kazi kubwa katika ngazi ya sanaa lakini vipato vya wasaanii wa fani hayo haviridhishi na wamekuwa ombaomba ndani ya jamii.

Alisema kuwa uamuzi wa taasisi hiyo kuwajali wasanii wakongwe ni moja ya kupongezwa kwa vile ni moja ya wigo na ubunifu mzuri ambao unahitaji kuendelezwa.

"Sisi wasanii wa zamani hali zetu zimekuwa ngumu kiuchumi hatuna hata sehemu za kuishi tunatangatanga tu na ulimwengu hadi siku yetu ya umauti zitakapofika za kuondoka duniani," alisema.

Fatma Issa msanii mkongwe na maarufu wa nyimbo za tarabu asilia, alisema kuwa wasanii wengi wa nyimbo za taarabu wa miaka ya nyuma wanaimba kwa upendo wa nchi yao, siyo kuweka tamaa ya kupata fedha ndiyo mana wengi wao kwa sasa hali zao zimekuwa duni.

Alisema kuwa wakati umefika kwa wasanii wa Zanzibar kuwa kitu kimoja katika kusaidiana hasa katika utunzi wa nyimbo zinazotoa ujumbe kwa jamii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**GLORIA NOVATUS MUSHI** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE 219171** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 16/10/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control Number **9910843031831.**

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**NURU ABDUL KAYUNGILO** anatangaza kupotelea na kadi za gari aina za **LANDCRUSER PICKUP** ZENYE MAJINA YA BULYANHULU GOLD MINE zenye namba za usajili **T833 BVD** TAARIFA YA POLISI: **PHQ/SHI/KAH/10834/2024.**NA **T256 BVC.** TAARIFA YA POLISI: **PHQ/SHI/KAH/10832/2024** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...83/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: JUMA MOHAMED GHONA wa MODEKO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA MOHAMED SULEIMAN GHONA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 Mwezi 12 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 14 mwezi 11 mwaka 2024

leo Tarehe ............

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA KONDOA**
**KANDA YA DODOMA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINA NA: 21/2020**
**(Linalotokana na shauri la Jinai 56/2020 la Mahakama ya Mwanzo Paranga)**

**MATAJI LESSI......................................MUOMBA RUFAA**

**DHIDI YA**

**MWALIMU SONGO....................................MJIBU RUFAA**

**KWA: MATAJI LESSI**
**POPOTE ALIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA 21/2020 MAHAKAMA YA WILAYA KONDOA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama ya Wilaya Kondoa, saa tatu kamili asubuhi (9:00) asubuhi siku ya tarehe 19.11.2024
**HIVYO BASI;** Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO;** hutofika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.
**IMETOLEWA:** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo 05 mwezi wa octoba, 2024.

.............................
HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA KONDOA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO V.**
**KITUO CHA MIKESE**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...9/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HAMISI JUMA MAJEMBE wa MKAMBARANI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA JAMILA IDDI MKOLAMASA**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

**Imetolewa leo tarehe 8 mwezi 10 mwaka 2024**

.............................................
**HAKIMU**

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**BERNAD KALAMU LYAKA** anatangaza kupotelea na kadi za gari aina ya scania 124 zenye namba za usajili **T 780 DLV** na hose na **T 955 DLU.** TAARIFA YA POLISI: **PHQ/SHI/KAH/10614/2024** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 25185/ 2024**
**In the matter of the Estate of the late SHUKURU PETER MOTAU of Bwawani Kisasa**
**Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**SARAH ABDALLAH GEREGEZA AND MICHAEL PETER MOTAU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**
.........................................................

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 Day of 11, 2024

.............................
1ST PETITIONER
...... ......
2ND PETITIONER
Presented for filling this 15 day of 10 2024
.......... ..............
RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No.27343/2024**
**In the matter of the Estate of the late MARY VENANCE KINTU of Ipagala**
**Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**NIPAEL VENANCE KINTU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 26 Day of 11, 2024
Date at Dodoma this 18TH Day of OCTOBER, 2024.

.............................
**PETITIONER**
**Presented for filling this 5 day of 11,2024**
.............................
**RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ISAKA AIVANI MUHUMPHA,** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA S.4732/0022 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA SHULE YA SEKONDARI CHONAMA MWAKA 2012. YEYOTE ATAKAEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/DOD/BAH/45096/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 174 YA MWAKA 2019**
**BAINA YA**

**ADOLPH LUKIZA KAHAMBA................................................MDAI**

**DHIDI YA**

**SETH GIDION ..........................................................MDAIWA**
**(NA WENZAKE 05)**

**KWA: SETH GIDION**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 13.01.2025 saa 3.00 asubuhi kwa ajili ya kutajwa na baadae kusikilizwa.
**ANGALIZO:** - Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kuendelea kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 08 ya Mwezi NOVEMBA, 2024

.....................................
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA TANZANIA

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 26850 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**TELESPHORY CHRISTOPHER BWAKILA. DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**

**1. SCHOLASTICA TELESPHORY MTONGA. 1st PETITIONER**
**2. ______________________________ 2nd PETITIONER**
**3. ______________________________ 3rd PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Under Rule 75 of Probate Rules and any other enabling Provision of the Law)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 26TH day of NOVEMBER.2024
Dated at MOROGORO this 13 day of NOV.2024

.............................
*PRINCIPAL/ SENIOR/ RESIDENT MAGISTRATE*
MOROGORO DISTRICT COURT
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ILEMELA**
**Kituo cha SANGABUYE**
**Mkoa MWANZA**
**SHAURI LA MADAI YA TALALA NA 12 YA 2024**
**MDAI.........ELIZABETH BUNDALA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA.........DEOGRATIAS BUNDALA**
**KWA: DEOGRATIAS BUNDALA – POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa kuwa mdai ameleta madai dhidi yako kwa hiyo shauri hili limepangwa kwa ajili ya kusikilizwa siku ya JUMANNE mnamo tarehe 19/11/2024 majira ya saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. L.H. NDOLEZI – HAKIMU MKAZI katika kituo cha Mahakama ya Mwanzo Ilemela Mkoa wa Mwanza. Kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo IJUMAA ya tarehe 15 NOVEMBA, 2024.

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARIKIMATAIFA

# Wananchi Senegal wapigakura kuwachagua wabunge

**DAKAR, Senegal**

WANANCHI nchini Senegal wamepiga kura kuwachagua wabunge huku ikielezwa kwamba hatua hiyo inatazamiwa kubainisha kama rais mteule wa nchi hiyo anaweza kufanya mageuzi makubwa.

Ilielezwa kuwa katika kura hizo zilizopigwa jana, zaidi ya wapigakura milioni saba waliojiandikisha watachagua wabunge 165 katika bunge la taifa, ambako chama cha Rais Bassirou Diomaye Faye kwa sasa hakina wingi wa kura.

Faye, ambaye alichaguliwa mwezi Machi, mwaka huu katika jukwaa la kupinga uanzishwaji, alisema hilo limemzuia kutekeleza mageuzi aliyoahidi wakati wa kampeni yake, ikiwa ni pamoja na kupiga vita rushwa, kupitia upya vibali vya uvuvi kwa makampuni ya kigeni na kupata sehemu kubwa ya maliasili za nchi idadi ya watu.

Pia ilielezwa kuwa Septemba, alivunja bunge linaloongozwa na upinzani, na kufungua njia ya uchaguzi wa ubunge wa haraka.

Ilielezwa kuwa chama chake kinakabiliwa na jukwaa la upinzani la Takku Wallu linaloongozwa na Rais wa zamani Macky Sall, pamoja na vyama vingine 39 vilivyosajiliwa na miungano.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa matokeo ya kwanza ya muda yanatarajiwa kujulikana asubuhi ya leo, lakini hesabu ya mwisho itachapishwa siku chache baadaye.

Vile vile, ilielezwa kuwa chama cha kisiasa cha Faye, PASTEF, kinahitaji angalau viti 83 ili kupata wingi wa wabunge. Huku wachambuzi wakisema ina nafasi kubwa ya kupata hilo, kutokana na umaarufu wake na tofauti ya ushindi wa Faye katika uchaguzi wa urais wa Machi.

Faye, 44, alichaguliwa kwa asilimia 54 katika duru ya kwanza, na kuwa kiongozi mwenye umri mdogo zaidi barani Afrika kuchaguliwa, chini ya wiki mbili baada ya kuachiliwa kutoka gerezani.

Kupanda kwake kumeonyesha kuchanganyikiwa kwa vijana wa Senegal na mwelekeo wa nchi, huku hisia ya kawaida ambayo ina idadi ya watu wadogo zaidi duniani na viongozi kadhaa wanaotuhumiwa kung'ang'ania madaraka kwa miongo kadhaa.

Wakati huo huo, ilielezwa kuwa zaidi ya asilimia 60 ya Wasenegali wako chini ya miaka 25 na asilimia 90 wanafanya kazi zisizo rasmi. Na kwamba Senegal imekumbwa na ongezeko la mfumuko wa bei katika miaka ya hivi karibuni, na hivyo kufanya iwe vigumu kwao kujimudu.

Nchi hiyo pia ni chanzo kikuu cha uhamiaji usio wa kawaida kwenda Ulaya, huku maelfu wakiondoka kila mwaka kwa boti mbovu za uvuvi kutafuta fursa za kiuchumi.

Kampeni za uchaguzi huo wa wabunge zilikumbwa na mapigano ya hapa na pale kati ya wafuasi wa vyama tofauti. Na kwamba makao makuu ya chama cha upinzani yalichomwa moto na mapigano yamezuka kati ya wafuasi katikati mwa Senegal katika wiki za hivi karibuni.

Ousmane Sonko, Waziri Mkuu wa nchi hiyo ambaye alimsaidia Faye kupata ushindi, alishutumu mashambulizi dhidi ya wafuasi wa PASTEF huko Dakar na miji mingine.

"Kila mzalendo waliyemshambulia na kujeruhi alipizwe kisasi sawia. Tutatumia haki yetu halali ya kujibu," aliandika kwenye X, kabla ya kukanyaga na kuwataka wafuasi wake kubaki watulivu katika hotuba baadaye siku hiyo.

**TRT**




Mmoja wa wananchi nchini Senegal akipiga kura katika uchaguzi wa kuchagua wabunge jana. **PICHA: MTANDAO**

# AU yashiriki mkutano wa G20

**RIO DE JENAIRO, Brazil**

MKUTANO wa 19 wa viongozi wa kundi la nchi 20 (G20) umeanza ambako ushiriki wa Tanzania umetajwa kusaidia kupata fedha za masharti nafuu na kupanua upatikanaji wa nishati safi, huku ikiwa ni mara ya kwanza kwa Umoja wa Afrika (AU) kushiriki.

Rais Samia Suluhu Hassan ni miongoni mwa viongozi wanaoshiriki katika mkutano huo wa kilele ulioanza leo mjini Rio De Jenairo Brazil, ambao utadumu siku mbili na kwamba ushiriki wake utakuwa ni mara ya kwanza kwa rais mwanamke kutoka Afrika kushiriki kwenye G20.

Ilielezwa kuwa AU inashiriki katika mkutano huo kama mwanachama kwa mara ya kwanza tangu kukubaliwa kama mwanachama wa kundi hilo Septemba 2023.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mahmoud Thabit Kombo, alisema kuwa Tanzania imepewa nafasi adhimu ya kukaa mezani na kundi ambalo linashikilia asilimia 75 ya biashara ya kimataifa na 85 ya pato la dunia.

"Huu ni ushuhuda wa kazi ya Rais wetu bila kuchoka katika azma yake ya kutoa njia za kuhamisha teknolojia na msaada wa kifedha kwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika," ilisema sehemu ya taarifa yake.

Alisema ushiriki wa Tanzania katika mkutano huo utasaidia juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya umaskini na njaa pamoja na kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

Waziri Kombo alisema ushiriki wa Rais Samia pia utaongeza mipango ya upishi safi na miundombinu mbadala muhimu kwa maisha endelevu.

Alisema mkutano huo utaipa Tanzania fursa ya kuvutia uwekezaji katika mipango ya usalama wa chakula kwa kukuza kilimo kinachozingatia hali ya hewa, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi hususan kwenye mifumo ya chakula na kuimarisha ustahimilivu wa kikanda.

Pia alisema ushiriki wa Rais Samia katika mkutano wa G20 unatarajiwa kuinua hadhi ya Watanzania katika ngazi ya dunia ili kukuza ushirikiano wa muda mrefu katika kufikia dira ya muda mrefu inayoendana na malengo ya maendeleo.

Alisema mkutano wa viongozi wa G20 utajadili vipaumbele vya maendeleo endelevu ambavyo ni ushirikishwaji wa kijamii na mapambano dhidi ya njaa na umaskini, mabadiliko ya nishati sambamba na kukuza maendeleo endelevu katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

"Maeneo haya yanawiana vyema na vipaumbele vilivyomo katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Tanzania 2025 na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050," alisema.

Aidha, G20 inaundwa na Argentina, Australia, Brazil, Canada, China, Ufaransa, Ujerumani, India, Indonesia, Italia, Japan, Mexico, Urusi, Saudi Arabia, Afrika Kusini, Korea Kusini, Uturuki, Uingereza na Marekani.

Hata hivyo, kundi hilo linaangalia ukuaji wa uchumi duniani, kushughulikia masuala muhimu ya kimataifa kama vile mabadiliko ya hali ya hewa, usalama wa nishati na maendeleo na kukuza ushirikiano wa kimataifa katika masuala muhimu kama vile biashara, fedha na uwekezaji.

## King Kiki kuagwa Leaders, kuzikwa leo Kinondoni

**Na Adam Fungamwango**

MWANAMUZIKI mkongwe nchini, Boniface Kikumbi Mwanza Mpango maarufu King Kiki, aliyefariki dunia usiku wa kumkia Ijumaa nyumbani kwake Mtoni kwa Aziz Ally, anatarajiwa kuzikwa leo kwenye makaburi ya Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Mtoto wa marehemu, Joseph Kikumbi, amesema mazishi ya mwanamuziki huyo yatafanyika leo na kama utaratibu utaenda kama ulivyopangwa, basi mashabiki wa muziki, ndugu, jamaa na marafiki watapata nafasi ya kumwaga kwenye viwanja wa Leaders Club, Dar es Salaam.

"Tumekaa kikao tutamzika Jumatatu, kukiwa na mabadiliko yoyote tutasema, tutampumzisha mzee wetu kwenye makaburi ya Kinondoni na kutafanya utaratibu aagwe viwanja wa Leaders," alisema Joseph.

Naye mtoto mwingine wa marehemu, Jesca Kikumbi, alisema baba yao alikuwa akisumbuliwa na tezi dume, pia saratani ilikuwa imepanda hadi kwenye ini. "Tumemuuguza sana mzee wetu, serikali ilitusaidia kumpeleka mpaka India, na siku za karibuni alirundishwa hospitalini, lakini baada ya kupata nafuu walimrejesha nyumbani," alisema Jesca.

King Kiki mwanamuziki mwimbaji, aliyefariki akiwa na miaka 77, alizaliwa Januari Mosi 1947, Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, baadaye akatokea kuwa mwanamuziki maarufu hasa nchini akiwa na bendi mbalimbali.

Mara ya kwanza alifika Tanzania akiwa na bendi ya Orchetra Fauvette mwanzoni mwa miaka ya 1970, akiwa na Freddy Ndala Kasheba na kutoa vibao mbalimbali kama 'Vivi, Nono na Kalimie, Zula, Jackline', lakini alirejea tena Zaire (sasa DRC), ambapo alikuja tena nchini katikati ya miaka hiyo, akijiunga na Maquis du Zaire, akatunga nyimbo nyingi kama 'Kasongo rudi Nyumbani, Maggie, Nimepigwa Ngwala', lakini aliihama bendi hiyo na kujiunga na OSS, 'Masantula Ngoma ya Mpwita', akitunga nyimbo kama 'Haruna Kaka, Ni kweli na zinginezo.

Baadaye aliunda bendi ya Orchestra King Kiki Double O, ambapo alitunga na kuimba nyimbo kama 'Lamanda, Kitoto Kaanza Tambaa, Dodoma Capital', kabla ya kwenda Zaita Musica na Ya Capital Wazee Sugu alipotunga kibao maarufu hadi leo 'Nzibola' maarufu kama 'Kitambaa Chaupe.'

# GAMONDI AWA KOCHA WA NANE KUTIMULIWA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

MIGUEL Gamondi amekuwa kocha wa nane kutimuliwa kwenye Ligi Kuu Tanzania hadi kufikia raundi ya 10 ya ligi hiyo.

Mwishoni mwa wiki hii, Klabu ya Yanga ilitangaza kumfuta kazi Gamondi bila ya kutaja sababu, lakini ni siku chache baada ya timu hiyo kupoteza michezo miwili ya Ligi Kuu, ikifungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC na kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa Tabora United.

Gamondi raia wa Argentina, aliyechukua kijiti hicho Yanga kutoka kwa Nasreddine Nabi msimu uliopita na kuipa ubingwa wa Tanzania Bara huku akiifikisha robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hadi anaoneshwa mlango wa kutokea msimu huu, alikuwa ameiongoza Yanga michezo 10, ikishinda minane na kupoteza miwili, ikikusanya pointi 24, ikiwa kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa ligi hiyo.

Mpaka sasa makocha wanane wameshatimuliwa kwenye Ligi Kuu kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kutofanya vema kwenye michuano hiyo na mingine pia.

David Ouma, raia wa Kenya, alikuwa wa kwanza kutimuliwa na Coastal Union na sababu ikiwa ni kutolewa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, timu hiyo sasa inafundishwa na Juma Mwambusi, sababu kama hizo zikamfanya pia Kocha raia wa Senegal, Youssouph Dabo kutimuliwa Azam FC, inayofundishwa na Mmorocco Rachid Taoussi kwa sasa.

Makocha wengine waliofutwa kazi kwenye Ligi Kuu ni Fikiri Elias wa KenGold sasa ikiwa chini ya Omari Kapilima, Paul Nkata wa Kagera Sugar, raia wa Uganda naye aliondolewa akaletwa Melis Medo, Mkenya Francis Kimanzi akaondolewa Tabora United, sasa iko chini ya Mkongomani, Anicet Kiazayidi, Mserbia, Goran Copunovic akatimuliwa Pamba Jiji, akachukuliwa Fred Felix Minziro, na Mwinyi Zahera wa Namungo aliyepewa kazi ya Mkurugenzi wa Ufundi, huku Juma Mgunda akichukua nafasi yake.

CHAMBUA...



Mshambuliaji na Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akiwachambua wachezaji wa Timu ya Taifa ya Ethiopia, na kutoa pasi ambayo ilimfikia Mudathir Yahya kabla ya kuzaa bao la pili kupitia kwa Feisal Salum 'Fei Toto', kwenye mechi ya Kundi H ya kuwania kufuzu AFCON 2025 iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Des Martyrs jijini Kinshasa, DR Congo. Stars ilishinda mabao 2-0. **MPIGAPICHA WETU**

# Kally kuwaongezea kasi wachezaji KMC

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu mpya wa KMC, Kalimangonga Ongalla, ameahidi kuwaongezea kasi wachezaji wa timu hiyo akisema hicho ndicho kitu ambacho wanaonekana kukikosa.

Akizungumza baada ya kuanza kazi yake hiyo mpya, akichukua mikoba ya Abdihamid Moallin, aliyeamua kuvunja mkataba mwenyewe, Kally alisema amekiangalia kikosi chake mazoezini na kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Simba uliochezwa Ijumaa, ameridhika na viwango vya wachezaji wake, lakini kuna baadhi ya matatizo ameyagundua.

"Katika mchezo dhidi ya Simba nilikuwa juu naangalia mechi, kuna vitu nimeviona vizuri, lakini vipo vichache ambavyo inabidi tuvirekebishe ila nimeridhika na kikosi. Kila kitu kinachofanyika kwenye uwanja wa mazoezi ni kizuri, lakini hatutakiwi kudorora, tunatakiwa kuongeza kasi, bado wanacheza taratibu, hili ndilo natakiwa kuanza nalo," alisema straika huyo wa zamani wa timu za Abajalo ya Sinza na baadaye Yanga.

Kocha huyo ambaye aliwahi kuinoa Azam FC, amewaahidi mashabiki wa KMC kuwa atatumia ujuzi na uzoefu wake wote ili kuhakikisha anashinda kwenye michezo ya Ligi Kuu.

"Nawaahidi mashabiki wa KMC nitafanya kila ninachoweza ili kushinda mechi za Ligi Kuu," alisema.

Moallin ambaye naye alitoka Azam FC kama Kally, aliiongoza KMC kwenye michezo 11 ya Ligi Kuu, akishinda minne, sare miwili na kupoteza mitano, huku akiiacha ikiwa nafasi ya saba kwa pointi 14.

Wakati taarifa zikisema kuwa huenda akatangazwa kuwa kocha msaidizi wa Yanga, juzi, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alikanusha akisema hawajafanya mazungumzo yoyote na kocha huyo raia wa Somalia, badala yake akasema kocha wao msaidizi ambaye tayari yupo hapa nchini na watamtangaza wakati wowote, anatoka nchini Poland.

Hata hivyo, Klabu ya KMC ilionekana kulalamika juu ya kuondoka kwa kocha wake huyo, ikidai ameshawishiwa na moja ya klabu hapa nchini, huku ikidai ilimshawishi wakati akiwa na mkataba kitu ambacho ni kosa kwa kanuni za mpira wa miguu na kuahidi kudai haki yao pindi litakapotokea hilo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAALAND ATASAINI CITY
MANCHESTER City wanazidi kuamini kuwa mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 24, atasaini mkataba mpya katika klabu hiyo ambao utamfanya kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika Ligi Kuu England. ***(Mirror)***

### MCATEE ATAKIWA WEST HAM
KLABU ya West Ham inatazamia kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City, James McAtee mwenye umri wa miaka 22, huku wakihofia kumpoteza fowadi wa Brazil, Lucas Paqueta (27), Januari. ***(Sun)***

### NISTELROOY ATAKA TIMU EPL
RUUD van Nistelrooy analenga kibarua kwenye Ligi Kuu England baada ya kuondoka kwake Manchester United. ***(Mirror)***

### LLORENTE ATAKIWA VILLA
KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery, anataka kuimarisha safu yake ya ulinzi kwa kumsajili mlinzi wa kati wa Hispania, Diego Llorente mwenye umri wa miaka 31, kutoka Real Betis katika dirisha la Januari, lakini mkataba wa muda mrefu wa beki huyo unaweza kuwa kikwazo. ***(Football Insider)***

### SANCET PIA ATAKIWA
ASTON Villa pia inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Oihan Sancet mwenye umri wa miaka 24, lakini hawana uhakika kama watatimiza masharti yake ya euro milioni 80. (£66.9m)***(Caught Offside)***

### ZIRKZEE AWINDWA
JUVENTUS inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Manchester United na Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 23, huku mustakabali wa fowadi wao raia wa Serbia, Dusan Vlahovic (24), ukiwa bado haujulikani. ***(CalcioMercato)***

### OSIMHEN BEI JUU
MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Victor Osimhen, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Galatasaray, atapatikana kwa euro milioni 75 msimu wa majira ya joto, kwa mujibu wa kifungu cha kuruhusiwa kuondoka kilichowekwa na Klabu yake ya Napoli kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### ISAK ANUKIA KUUZWA
KLABU ya Newcastle United inaweza kulenga kumuuza mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25 na kutumia fedha hizo kumnunua mbadala wake. ***(Football Insider)***

### TAH HATASAINI
MLINZI wa kati wa Ujerumani, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 28, hatatia saini mkataba mpya na mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bayer Leverkusen na anataka kuhamia Bayern Munich au Barcelona kwa uhamisho wa bila malipo. ***(Sky Sports)***

### SKRINIAR KUONDOKA PSG
BEKI wa Paris St-Germain, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari kurejea Italia na kutua pale Juventus, wakati huu Mslovakia huyo akiendelea kutatizika kupata muda wa kucheza katika klabu hiyo ya Ufaransa. ***(La Gazzetta dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO SASA ADOKEZA MPANGO WA KUSTAAFU

● ● ● Natimiza miaka 40 hivi karibuni, ikibidi itokee mwaka mmoja au miwili ijayo, lakini sijui...

**LISBON, Ureno**

CRISTIANO Ronaldo alidokeza mpango wake wa kustaafu soka baada ya kuweka rekodi mpya ya kushinda mechi nyingi zaidi za kimataifa kwa soka la wanaume, Ijumaa iliyopita.

Ureno iliifunga Poland mabao 5-1 huku yeye akitikisa nyavu mara mbili na kuiwezesha kutinga robo fainali ya Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Ulikuwa ushindi wa 132 wa Ronaldo katika mechi za kimataifa, akimpita mchezaji mwenzake wa zamani wa Real Madrid, Sergio Ramos, ambaye alishinda mechi 131 akiwa na Hispania.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Ronaldo mwenye umri wa miaka 39, alisisitiza kwamba umakini wake unabaki kwenye kufurahia soka lake licha ya kuwapo kwa wasiwasi juu ya kustaafu.

"Nataka tu kufurahia mwenyewe," alisema.

"Kupanga kustaafu? Ikiwa itabidi itokee katika mwaka mmoja au miwili ijayo, lakini sijui. Ninatimiza miaka 40 hivi karibuni.

"Natamani sana kufurahia, mradi nijisikie kuwa na motisha na kuendelea kucheza. Siku ambayo sijisikii, nitastaafu."

Ronaldo aliongeza kuwa hana nia ya kwenda kuwa kocha baada ya kutundika daluga zake.

"Sijioni nikiisimamia timu; hiyo haipo katika mipango yangu," alisema.

"Mustakabali wangu upo katika maeneo mengine nje ya soka, ingawa muda utaonesha nini kitatokea."

Ureno itacheza na Croatia katika mchezo wao wa mwisho wa kundi la Ligi ya Mataifa ya UEFA leo Jumatatu.

## Osimhen anogewa na Galatasaray

**ISTANBUL, Uturuki**

VICTOR Osimhen hana nia ya kukatiza mkopo wake na Galatasaray wakati wa dirisha la usajili la Januari.

Napoli walitaka kumuuza kabisa Osimhen wakati wa majira ya joto na Chelsea walifanya mazungumzo hadi saa ya mwisho, lakini wakashindwa kufikia makubaliano.

Huku mshambuliaji huyo akiwa nje ya kikosi cha Napoli, Osimhen alitia saini ya mkopo wa miezi 12 kwa miamba hiyo ya Uturuki, Galatasaray.

Ripoti zimedokeza kuwa Chelsea inataka kufufua nia yao ya kumnunua Osimhen wakati wa dirisha la majira ya baridi, lakini kwa mujibu wa ripoti, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Nigeria hataki kuondoka Galatasaray mapema.

Inasemekana Osimhen, ambaye amefunga mabao nane na kutoa asisti nne katika mechi tisa msimu huu, anafurahia muda wake huko Istanbul, baada ya kujidhihirisha kuwa kipenzi cha mashabiki na bado hafikirii chochote zaidi ya hapo.

Galatasaray inatarajiwa kujaribu kumsajili Osimhen kabisa msimu ujao wa majira ya joto, wakiamini kuwa atavutiwa na mpango wao, lakini Napoli wanapanga kudai angalau euro milioni 75 kitu ambacho kitafanya mpango huo kuwa mgumu.

Hilo linaweza kufungua milango kwa Chelsea ambao tofauti na Galatasaray, wana uwezo wa kugharamia uhamisho huo.

Chelsea ilikataa kusajili mshambuliaji mpya baada ya harakati zao za kumnasa Osimhen kushindikana.

Kocha Enzo Maresca amedumisha imani yake kwa Nicolas Jackson, ambaye amefunga mara sita katika mechi 11 za Ligi Kuu England, huku chaguo la akiba Christopher Nkunku akiwa na mabao tisa katika michezo saba.

## Raya: Arsenal ina nafasi ubingwa EPL



**LONDON, England**

GOLIKIPA wa Arsenal, David Raya, amewataka wachezaji wenzake kutokata tamaa wanapojaribu kujiimarisha katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England (EPL), msimu huu.

Michezo minne bila ushindi kwenye Ligi Kuu umewaacha 'Washikabunduki' hao wakipitwa pointi tisa na vinara, Liverpool.

Miamba hao wa Kaskazini mwa London, wamekuwa wapinzani wakuu wa Manchester City katika misimu michache iliyopita na Raya amesisitiza kuwa timu yake ina kile kinachohitajika ili kujikokota tena kwenye mchuano huo.

Aliliambia gazeti la Mundo Depotivo kuwa: "Tumeonesha mwaka jana na msimu huu, japo hatujaanza tulivyopenda, hasa michezo miwili iliyopita kutokana na mazingira ya mechi hizo.

"Hatupaswi kutoa visingizio na lazima tusonge mbele. Tulistahili zaidi dhidi ya Chelsea na Newcastle United, lakini tutaendelea katika mkondo huo huo, kurekebisha makosa na kuangalia mbele na kundi zuri sana ambalo tunaweza kufanya chochote. Tutakuwa kwenye safu ya kupambana kutwaa Ligi Kuu."

Arsenal walipambana na Man City na Liverpool na walikuwa mbele katika mbio za ubingwa mwishoni mwa Aprili mapema mwaka huu, lakini kupoteza dhidi ya Aston Villa kulifanya waondoe nafasi yao ya kwanza na hatimaye kumaliza kama washindi wa pili.

Kazi kubwa inahitajika kukaribia nafasi hiyo msimu huu na watacheza na Nottingham Forest, West Ham United na Manchester United katika mechi zao tatu za kwanza za ligi baada ya mapumziko ya Novemba, huku pia wakihitaji kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya watakapocheza dhidi ya Sporting CP baada ya kufungwa bao 1-0 na Inter Milan.



# WATANO KUMSAIDIA AMORIM MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imethibitisha kuwasili kwa makocha watano ambao watafanya kazi benchi la ufundi pamoja na Kocha Mkuu, Ruben Amorim.

Kocha huyo wa zamani wa Sporting CP amewachukua baadhi ya wasaidizi wake ambao walimsaidia kushinda mataji mawili ya Ligi Kuu Ureno wakati wa utumishi wake nchini humo.

Taarifa ya klabu zimethibitisha kuwa Carlos Fernandes, Jorge Vital, Adelio Candido, Emanuel Ferro na Paulo Barreira wote wamejiunga na United huku timu hiyo ikitarajia kurejea kutoka kwenye wakati mgumu wa kutofanikiwa katika kipindi cha Erik ten Hag.

Wataungana na kiungo wa zamani wa United, Darren Fletcher na Andreas Georgson kama makocha wa kikosi cha kwanza.

Benchi jipya linakabiliwa na mtihani wake wa kwanza wakati watakapocheza dhidi ya Ipswich Town Jumapili wiki hii.

Wakati huo huo, Bruno Fernandes amerejea haraka Manchester kukutana na kocha wake mpya Amorim licha ya Ureno kuwa na mchezo mwingine dhidi ya Croatia katika Ligi ya Mataifa ya UEFA leo Jumatatu.

Fernandes aliruhusiwa mapema kutoka kambini baada ya kuoneshwa kadi ya njano wakati Ureno iliposhinda mabao 5-1 dhidi ya Poland Ijumaa na kumfanya afungiwe safari ya kwenda Zagreb.

HABARI MICHEZO

# FADLU APAGAWA KIPAJI CHA MPANZU, AWAITA MASHABIKI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili likikaribia kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amewaambia wanachama na mashabiki wa Simba kuwa, wakae tayari kumuona mchezaji mpya, Elie Mpanzu, akisema ataongeza kitu ndani ya kikosi chake kutokana na kipaji kikubwa alichonacho, huku akimtabiria makubwa.

Kocha huyo raia wa Afrika Kusini, alisema jana kuwa anaamini kutokana na kipaji alichonacho, atafunga mabao mengi na kuwasaidia wenzake kuwapa pasi za mwisho kwa ajili ya kupambania nembo ya klabu hiyo.

Ijumaa iliyopita, mchezaji huyo alicheza kwa dakika kadhaa kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya KMC, uliochezwa Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam na kutoka sare ya bao 1-1, lakini haikuhudhuriwa na mashabiki.

"Tunategemea kuwa atafunga sana na atatengeneza nafasi nyingi kwa wenzake, tunategemea atafiti kwenye kila mfumo wetu, tunamtegemea sana Mpanzu kuleta upinzani ndani ya kikosi," alisema kocha huyo.

Mpanzu ataanza kuitumikia Simba kwenye mashindano rasmi Desemba 15 wakati timu hiyo itakapocheza mechi yake ya raundi ya tatu ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia, utakaopigwa, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, huku akitarajiwa kuonekana kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu itapovaana na KenGold, Desemba 18, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

"Mpanzu ni mchezaji wa kipekee sana, tumekaa naye vikao vingi kuona ni sehemu gani anaweza kuzoea na kuwa huru akicheza uwanjani, tunataka azoee mipango yetu ajue nini cha kufanya akiwa na mpira, nafasi ipi achukue uwanjani akiwa na mpira na hata asipokuwa nao.

"Tumekaa naye vikao kuangalia ni namna gani anaweza kushambulia kulingana na wapinzani wetu wanavyocheza, nini tunafanya tunapokuwa tuna mpira, muda ambao hatuna, kinachobaki ni yeye mwenyewe kujiweka sawa na kuzoea mifumo yetu kwa kuwa bado hajaanza kucheza michezo ya mashindano, ila hii michezo ya kirafiki itamsaidia," alisema kocha huyo.

Mabosi wa Simba walimpa mkataba winga huyo raia wa Jamhuri ya Kidemkorasi ya Congo, kabla ya dirisha dogo la usajili.

Awali, Mpanzu, alikuwa asajiliwe na Simba kipindi cha dirisha kubwa, lakini dili liliharibika baada ya kutimkia nchini Ubelgiji kwenda kufanya majaribio katika Klabu ya Genk, ambayo hayakufanikiwa.

Baada ya kutofanikiwa na kumaliza mkataba wake na AS Vita, Simba ilirejea kwenye meza ya mazungumzo na mchezaji huyo, ikampa mkataba haraka kabla ya dirisha dogo ili kuepuka dili hilo kuvunjika tena.




Winga mpya wa Simba, Elie Mpanzu, akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa KMC FC, kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa KMC Complex na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: SIMBA**

## Msimu aukubali muziki wa KMKM

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAAFANDE wa KVZ FC, wamejikuta wakibanwa mbavu na Wanamaji KMKM SC kwa kutoka sare tasa katika mechi ya mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa 11.

Mchezo huo ulichezwa juzi Jumamosi katika dimba la Mau A majira ya saa kumi alasiri na kuhudhuriwa na mashabiki kiasi wa timu zote mbili.

Akizungumza na gazeti hili juzi Kocha wa KMKM SC, Ame Msimu, alisema licha ya kutotarajia matokeo hayo ya sare, lakini tangu hapo awali alijua mchezo huo utakuwa mgumu.

Alisema kipindi cha kwanza timu yake ilicheza vizuri, lakini walishindwa kupata bao licha ya kutengeneza nafasi nyingi.

Msimu alisema wapinzani wao walikuwa bora katika kipindi cha pili ambacho walimiliki mpira na kuwashambulia, lakini umakini wa safu yake ya ulinzi uliweza kuhimili mashambulizi hayo.

"Ulikuwa mchezo mgumu sana, kwa kuwa kila timu ilishuka uwanjani lengo likiwa ni kupata alama ambazo zitamweka juu, lakini haikuwa bahati na tumegawana alama," alisema.

Aidha, alisema kuwa bado timu yake inahitaji kupata ushindi wa alama tatu kutokana na matokeo ya michezo iliyopita ya kupata sare na kufungwa.

Alisema anaenda katika uwanja wa mazoezi kwa kuyafanyia kazi makosa ambayo mara kwa mara yanajitokeza katika timu yake.

Hata hivyo, aliwataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kutoa hamasa kwa timu yao ili kuwapa moyo wachezaji wao hasa katika wakati huu ambao hawana mlolongo mzuri wa matokeo.

Kwa matokeo hayo KMKM SC imekwea nafasi moja juu ikitokea ya saba hadi ya sita na alama zake 17 wakati Maafande wa KVZ FC wakiwa nafasi ya tano na alama zao 18.

## Ramovic atamba kuifahamu Simba

INATOKA UK. 24

yake sana.

"Naifahamu pia Simba kwa sababu kocha wao, Fadlu ni rafiki yangu, alikuwa mwalimu wa Orlando Pirates wakati huo wote tukiwa Afrika Kusini," alisema.

Kocha huyo ataanza mtihani wake wa kwanza Novemba 26, mwaka huu, atakapokiongoza kikosi cha Yanga kucheza mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Gamondi aliifikisha timu hiyo hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita na kutolewa kwa mbinde na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwa mikwaju ya penalti 3-2, Aprili 5, mwaka huu, huko Sauzi.

Hatua hiyo ya ‚matuta' ilifikiwa baada ya suluhu mbili, ya kwanza ikipatikana kwenye mchezo wa awali uliochezwa, Machi 30, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kocha huyo pia ana kazi nyingine ya kuulinda ubingwa aliouchukua Gamondi msimu uliopita, ambaye ametemwa akiwa kwenye nafasi ya pili ya msimamo msimu huu akiwa ameiongoza kushinda michezo 10, kushinda minane na kupoteza miwili dhidi ya Azam FC na Tabora United, ambayo inadhaniwa kwa kiasi kikubwa kuwa chanzo cha kutwaa kazi kwa Muargentina huyo.

## Morocco: Lazima tuifunge Guinea

INATOKA UK. 24

kazi kwani wanakwenda kucheza mchezo mgumu zaidi, lakini akiwatoa wasiwasi Watanzania kuwa watafanya kila linalowezekana kuwezesha kupata matokeo ya ushindi.

"Mechi ilikuwa nzuri, ilikuwa ngumu, lakini tumeshinda, tumefurahi ila kazi bado inaendelea kwa sababu tuna mchezo mwingine mgumu dhidi ya Guinea. Tunahitaji ushindi tu ili tufuzu, tunaomba Watanzania tuungane kwa pamoja, sisi ndani ya uwanja tutapambana kwa ajili yao," alisema.

Yalikuwa ni mabao ya Msuva na Feisal Salum ‚Fei Toto' yaliyofanya Stars kufikisha pointi saba, ikihitaji kuifunga Guinea tu yenye ponti tisa, ili kufikisha pointi 10 na kufuzu AFCON kwa nafasi ya pili, baada ya DR Congo kuwa timu ya kwanza kwenye Kundi H kufuzu fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

# Michezo

Jumatatu Novemba 18, 2024

Nipashe


**Watano kumsaidia Amorim Man United**

UKURASA 22



KESHO TENA...



Winga wa Taifa Stars, Simon Msuva (watatu kushoto), akipongezwa na wachezaji wenzake baada ya kuifungia timu hiyo bao la kwanza wakati ikishinda mabao 2-0 dhidi ya Ethiopia kwenye mechi ya Kundi H ya kuwania kufuzu AFCON 2025 iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Des Martyrs jijini Kinshasa, DR Congo. Kesho Stars itajitupa Uwanja wa Benjamin Mkapa kusaka ushindi dhidi ya Guinea ili kufuzu fainali hizo. **MPIGAPICHA WETU**

# RAMOVIC ATAMBA KUIFAHAMU SIMBA

Ataka umoja mashabiki Yanga, huku pia akieleza anavyomfahamu kocha Fadlu na kwamba...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Yanga, Sead Ramovic raia wa Ujerumani, ameonesha furaha kubwa kupata nafasi ya kuifundisha timu kubwa kama hiyo, huku akisema anaifahamu sana Simba na kumtaja kocha wa timu hiyo, Fadlu Davids, kuwa ni rafiki yake.

Akizungumza kwa mara ya kwanza jana baada ya kutangazwa kuwa Kocha Mkuu, akichukua nafasi ya Miguel Gamondi, Sead aliyetokea Klabu ya TS Galaxy ya Afrika Kusini, aliwataka wanachama, mashabiki, wapenzi, viongozi na wao kama makocha kuungana kwa pamoja ili kufikia malengo.

"Ni heshima kubwa sana kuwa hapa kuifundisha hii timu, ni klabu kubwa sana yenye wachezaji wenye vipaji vikubwa, na ni fahari kuwaongoza na kuendeleza mafanikio ya klabu hii yenye mataji mengi, na nia yangu ni kufanya kila ninachoweza ili kulinda yaliyopo na kuleta mengine mapya," alisema kocha huyo.

Alisema alikiona kikosi hicho nchini Afrika Kusini kilipokwenda kucheza michezo ya kirafiki ya kimataifa kabla ya kuanza msimu mpya.

"Nilikiona kikosi cha Yanga kilipocheza na FC Augsburg ya Ujerumani, wakacheza na sisi pia TS Galaxy, niliona kuwa ni timu iliyokuwa na wachezaji wenye vipaji sana, lakini pia naona fahari sana kuifundisha timu hii yenye mashabiki wengi sana nchini, siwezi kusema nalifahamu sana soka la Tanzania, lakini najua kuwa Yanga ndiyo timu bora kwa sasa hapa nchini," alisema.

Pamoja na hayo, alisema anaifahamu sana timu ya Simba, huku pia akisema kocha wa sasa wa timu hiyo, Fadlu ni rafiki

INAENDELEA UK. 23

## Morocco: Lazima tuifunge Guinea

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa, Taifa Stars, Hemed Suleiman ,Morocco', amesema ushindi wa mabao 2-0 walioupata dhidi ya Ethiopia juzi nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, umewapa chachu na nguvu ya kushinda mchezo wao wa kesho dhidi ya Guinea, akiongeza kuwa hakuna kiswahili kingine tena zaidi ya kuichapa timu hiyo ili Tanzania ifuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika, (AFCON) 2025.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Des Martyrs uliopo Kinshasa, ambako Ethiopia waliamua kuchezea mechi yao ya nyumbani huko kutokana na viwanja vyao kushindwa kukidhi vigezo vilivyowekwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Morocco, alisema hakuna muda wa kupoteza wala kufurahia matokeo hayo, badala yake wanajipanga kwa mchezo ujao dhidi ya Guinea ambao ndio utatoa hatima ya Tanzania kwenda nchini Morocco kwa ajili ya fainali hizo.

Sasa tunahitaji kushinda mechi ya mwisho, hakuna kiswahili kingine, ili tufuzu ni lazima tushinde, tunarudi kwenye uwanja wa mazoezi ili tujipange na yale mapungufu yaliyoonekana tuyarekebishe, tunajua mechi itakuwa ngumu sana, ila ushindi huu dhidi ya Ethiopia umetutia chachu, tutakuwa imara zaidi katika mchezo ujao kuliko huu," alisema kocha huyo.

Akizungumzia mazingira ya mchezo wenyewe, alisema haikuwa rahisi kutokana na falsafa ya mpira wa Ethiopia ambao mara zote ni kumiliki mpira, hivyo ilibidi wafanye kazi ya ziada.

"Tulijua kuwa mechi itakuwa ngumu kwa sababu Ethiopia ni timu ambayo inajua sana kumiliki mpira, ndiyo uchezaji wao, ndiyo falsafa yao ya miaka yote, mkakati tulioingia ni kuzuia njia zao na tulitaka kuimaliza mechi mapema, na iliwezekana kwani tulitengeneza nafasi nyingi hatukuzitumia, ni mbili tu ndiyo tulifanikiwa kufunga," alisema.

Naye mfungaji wa bao la kwanza, Simon Msuva, alisema wamefurahi kupata ushindi, lakini bado wana

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >